

“ UCHANGANUZI WA KISHAZI ELEZI CHA KISWAHILI SANIFU

MTAZAMO WA KIMOFOSINTAKSIA ”

NA

MARGARET WANJALA MWACHANYA

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO

KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

University of NAIROBI Library



0478428 6

2009

UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu. Kwa ufahamu wangu wote, nina uhakika, kazi kama hii haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote kile.




22/10/09

MARGARET WANJALA MWACHANYA
(MTAFITI)

TAREHE


Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii Chuo Kikuu cha Nairobi.



29/10/09

For PROF. KITHAKA WA MBERIA.
(MSIMAMIZI)

TAREHE



30/10/09

BI.MARGARET NJUGUNA
(MSIMAMIZI)

TAREHE



29/10/2009

DKT.HELGA SCHROEDER
(MSIMAMIZI)

TAREHE

TABARUKU

Nilikosa pendo lake kwa kupokonywa na yule ambaye akishachukua haregeshi tena. Tangu siku hiyo siwezi kupenda, naogopa kupenda na kila nifikiriapo penzi hushtuka kama aliyekanyaga ganda la nyoka. Mungu mwenye enzi ailaze roho yake mahali pema peponi.

Tulipendana bila ya kufahamu kuwa mapenzi hayo ni kwa kuwa mmoja wetu alikuwa mgeni wa mwenziwe. Tasnifu hii naitabarukia marehemu dadangu mpendwa:

RUSSIANA WONGE MWACHALA

SHUKRANI

Wasoamini na waamini. Msema kweli si mwongo. Hakuna ajiwezaye. Kila mmoja wetu huwa na ndoto za maishani. Ndoto za wengi zimebaki kuwa ndoto za kuota na wala hazijawahi kutekelezwa. Ingingekuwa ni usaidizi wa wengi nitakao wataja na ambao sitawataja kwa sababu za kibinafsi, hakika kozi hii ingalinikalia ngumu sana. Natoa shukrani zangu kwa moyo mkunjufu kwa wote wafuatao: Kwanza namshukuru Maulana kwa kunijalia fursa ya kutekeleza ndoto yangu. Shukrani zangu zisizo na kifani ni kwa Taasisi ya Kuajiri Waalimu. Walinipatia likizo ya kurudi masomoni baada ya kufunza kwa miaka miwili tu.

Tatu natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu: Prof. Kithaka Wa mberia, Bi. Margaret Njuguna na Dkt. Helga Schroeder kwa kunisimamia, kunielekeza na kuisoma kazi yangu kwa moyo mkunjufu. Mpaka wa leo sijui ningeshika wapi na kujimudu vipi? Kweli ahangaikaye nawe usimhangaishe! Kama asingalikuwa Dkt. Helga Schroeder aliyenisimamisha nilipokuwa karibu kuanguka, sijui ningalikuwa leo nasimulia nani na yapi? Ndiye aliyenitia motisha ya kuisoma, kuielewa na kuitumia nadharia ya X-baa kwa mujibu wa Umilikifu na Masharti katika utafiti wangu.

Siwezi kusahau wahadhiri na wafanyikazi wote wa Chuo Kikuu Cha Katoliki cha Afrika Mashariki na ya Kati.

Msingi imara na wa kudumu mlionijaza nao teletele nilipokuwa nikisomea shahada yangu ya kwanza. Kama sio msingi huu imara, sio kielimu tu bali hata kumtegemea Jehova maishani, nisingaliweza kufika nilipo.

Nimefahamu fika kuwa njia ya kufahamu ni ndefu na wala haina kikomo. Hawajakosea waliponena “palipo na wazee hapaharibiki jambo”. Shukrani zangu bado nazitoa kwa wahadhiri wangu walionifaa sana katika kulibingirisha gurudumu hili: Dkt. Olali T.M., ndiye aliyenisomea matini ya nadharia niliyotumia. Prof. Abdulaziz M. H, Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt. John Habwe, Dkt. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Alfred Burugeya.

Wenzangu tuliobiringisha gurudumu hili pamoja, kwanza nawashukuru kwa kujuana nao pamoja na kufanya urafiki nanyi. Zaidi ni kwa usaidizi nilioupata kutoka kwenu. Geofry Mkabane licha ya kuwa na kazi na majukumu mengi yaliyokusonga, ulinipiga jeki wakati chombo kilipokaribia kwenda mrama, sijui ningalimsimulia nani hasa wakati tulipokuwa tunatayarisha pendekezo la utafiti. Uliweza kuchukua mda wako kunielezea na kunifafanulia mambo pale nilipohitaji usaidizi wa dharura. Wengine tuliongoa nanga pamoja ni: Mary Ndung'u, Lina Akaka, Josephine Mulila, Gitonga na Nyaga. Wote hawa ni nyongeza ya idadi ya marafiki zangu nitakaowahifadhi maishani mwangu.

Siwezi kosa kumtaja hapa John Mwagambo. Ulinipa tarakalishi yako kila nilipoihitaji, hasa pale maji yalipokuwa yamepita shingoni. Labda tasnifu hii ingalikwama kama si kwa usaidizi wako. Julius Kirigha uliyenichapishia na kunitolea nakala za utafiti wangu. Samson Adekhera hata sijui ningalishika wapi? Rabii na akuzidishie hasa hekima ipitayo fahamu za mwanadamu. Marafiki zangu wote ambao nikianza kuwataja tasnifu itakuwa pana zaidi. Nilibaki kuwahisi uwepo wenu kwa hali na mali: Petero Maina, Peter Ingolan na wengine wengi sana.

Lazima nitaje Edmond Kiriga, Herrine Tots na Oswald Mghanga kwa kunitia joto kila ubaridi wa safari nzito nilipouhisi. Mwisho kabisa ni kwa wazazi wangu. Walionipa mshawasha wa kupenda na kuhitaji sio tu masoma lakini upeo wa elimu. Babangu ni mzazi aliyeogopa sana kutofaulu. Uoga huu wa babangu ulinipa changamoto ya kutia bidii masomoni mwangu. Nilifahamu tangu utotoni kuwa elimu ni ufunguo wa maisha.

ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA ZILIZOTUMIKA

KBn	-	kibainishi
KE	-	kirai elezi
Kih	-	kihusishi
Kij	-	kijalizo
KKBn	-	kirai kibainishi
KN	-	kirai nomino
KT	-	kirai Tenzi
Ktmb	-	kitambulishi
KU	-	kirai cha uambishaji kisarufi
KV	-	kirai Vumishi
n.k.	-	na kadhalika
Nj	-	njeo
Spes.	-	spesifaya
T	-	kitenzi
Tksd	-	kitenzi kisaidizi
TY	-	tafsiri yetu
U ¹	-	uambishaji wa baa- moja
U ¹¹	-	uambishaji wa baa- mbili
UK	-	ukanishi
UM	-	Umilikifu na Masharti
UPT	-	upatanisho

xyz^*	-	tazama ufafanuzi hapa chini
$*xyz$	-	si sahihi
\emptyset	-	kapa
$\{ \}$	-	mipaka ya mofimu
$;$	-	inaweza kubadilishwa nafasi
$*$	-	zaweza kuwa nyingi
X^0	-	sarufi
$X1$	-	mvurumisho wa kiwango cha juu kabisa
$X11$	-	mvurumisho wa kiwango cha juu zaidi.

TAFSIRI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

Agumenti	argument
Amri	commands
Athari	trace
Kanuni ya skema	rule schema
Kifundo	code
Kijalizi	complementizer
Kijalizi cha utoano	invert complementiser
Kijalizo	complement
Kirai cha x	xphrase
Kishazi	clause
Kishazi jalizi	complement clause
Kishazi tegemezi	dependent clause
Kitambulishi	marker
Kitenzi kisaidizi	inverted auxiliary
Leksikoni	lexicon
Mantiki	logic
Mvurumisho	projection
Sarufi bia	universal grammar
Spesifaya	specifier
Uambatani	coordination
Uambishaji	inflection

Uambishaji kisarufi	inflectional grammar
Uambishaji kisarufi	inflectional phrase
Ujenzi miundo	structure building
Umbo	configuration
Umilisi	competence
Utegemezi	subordination
Utendaji	performance
Uundi husishi	prepositional phrase
Vishazi bebwa	embedded clauses
Vishazi dondoshi	elliptical clauses
Vishazi rejeshi	relative clauses
Vishazi unganishi	co-ordinated clauses
Vishazi vidhibitishi	confirmatory clauses
Vishazi vihisishi	interjective clauses
Vishazi vikuu / huru	superordinate clauses
Vishazi vumishi	adnominal / adjectival clauses
Wasilisho	presentation

YALIYOMO

UNGAMO	i
TABARUKU	ii
SHUKRANI.....	iii
ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA ZILIZOTUMIKA	vi
TAFSIRI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA.....	viii
SURA YA KWANZA	3
UTANGULIZI	3
1.1. PENGO LA KUZIBA.....	4
1.2. MADHUMUNI YA UTAFITI	5
1.3. . SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII	6
1.3. UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI	7
1.4. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....	19
1.5. MBINU ZA UTAFITI	26
SURA YA PILI.....	27
KISHAZI ELEZI CHA KISWAHILI SANIFU	27
UTANGULIZI	27
2.1 DHANA YA VISHAZI	27
2.2 AINA YA VISHAZI ELEZI.....	32
2.2.1 Kishazi elezi cha wakati.....	33
2.2.2 Kishazi elezi cha mahali	36
2.2.3 Kishazi elezi cha masharti na ukubalifu	38
2.2.4 Kishazi elezi cha sababu	40
2.2.5 Kishazi elezi cha hali	42
2.2.6 Kishazi elezi cha matokeo	46
2.2.7 Kishazi elezi cha namna/jinsi na ulinganishi	48
2.2.8 Vishazi elezi vya kukubali	51
2.2.9 Vishazi elezi vya nia/ kusudi	53
2.2.10 Vishazi elezi vya kiwango	54
2.3 HITIMISHO.....	56
SURA YA TATU	58
UTUMIZI WA NADHARIA YA X- BAA KATIKA	58
UCHANGANUZI WA VISHAZI ELEZI KWA.....	58
MUJIBU WA NADHARIA YA UMILIKIFU NA	58
MASHARTI.....	58
UTANGULIZI	58
3.1 KISHAZI ELEZI CHA WAKATI.....	58
3.2 KISHAZI ELEZI CHA MAHALI	60
3.3 KISHAZI ELEZI CHA MASHARTI NA UKUBALIFU	62
3.4 KISHAZI ELEZI CHA SABABU	68
3.5 KISHAZI ELEZI CHA HALI	69
3.6 KISHAZI ELEZI CHA MATOKEO	73
3.7 KISHAZI ELEZI CHA NAMNA/JINSI NA ULINGANIFU	75
3.8 KISHAZI ELEZI CHA KUKUBALI	77

3.9	KISHAZI ELEZI CHA NIA/ KUSUDI.....	79
3.10	HITIMISHO.....	80
SURA	YA NNE.....	81
4.1	HITIMISHO.....	81
4.2	PENDEKEZO.....	84
MAREJELEO	85

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu. Kiswahili sanifu ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili zinazozungumzwa Afrika Mashariki na sehemu za Afrika ya kati.

Kuna lahaja nyingi za Kiswahili zilizoenea Afrika Mashariki kuanzia Mogadishu nchini Somalia kupitia Kenya, Tanzania, Msumbiji, na Zaire. Pia nchini Kongo na Uganda Kiswahili huzungumzwa. Baadhi ya lahaja hizi ni: Kitukuu, Kisiu, Kipate, Kiamu, Kimvita, Kimrima, Kichichifundi, Kivumba, Kingare, Kipemba, Kiunguja, Kimtang'ata, Kitumbatu, Kihadimu, Kingazija na Kingwana.

Baada ya kusoma kazi nyingi za Kiswahili tulipitia tasnifu ya Mwalili (2008) aliyefanya uchanganuzi juu ya kishazi nomino. Katika pendekezo lake, alipendekeza vishazi elezi na vishazi rejeshi kufanyiwa utafiti. Kutokana na pendekezo la Mwalili, niliamua kufanya utafiti wa vishazi elezi.

1.1.PENGO LA KUZIBA

Baada ya kudurusu majarida,vitabu na tasnifu tuligundua ya kwamba wasomi wa Kiswahili mara nyingi hutegemea kupata habari za isimu kutoka katika vitabu vya Kiingereza. Ukweli ni kwamba habari za isimu ni habari za isimu hata zikiwa katika lugha ipi! Lakini lugha hizi mbili yaani Kiswahili na Kiingereza zinatofautiana. Tofauti tunayozungumzia hapa ni kwamba, Kiingereza ni lugha ambishimchanganyo na Kiswahili ni lugha ambishibainishi Mgullu, (1998). Muundo wa Kiswahili sanifu una uhuru wa kubadilisha kategoria zake katika tungo bila ya kubadilisha maana iliyokusudiwa. Hii ni kumaanisha ya kuwa kiima, kiarifu, yambwa na kitenzi wakati mwingine huweza kubadilisha nafasi zao katika tungo bila ya kubadilisha maana ya awali.

Hivyo basi tunapopata mifano kutoka lugha ya Kiingereza huenda ikakosa kukidhi mahitaji ya lugha ya Kiswahili hasa kisintaksia. Kwa kuwa tuligundua hakuna kazi yoyote ya kishazi elezi katika Kiswahili sanifu, ndio maana utafiti huu utashughulikia kishazi elezi katika Kiswahili sanifu.

1.2.MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti huu, tunatarajia kupata majibu ya maswali yafuatayo:

- i) Je, kuna aina ngapi ya vishazi elezi katika lugha ya Kiswahili?
- ii) Je, kanuni ya ukaguzi sifa katika nadharia ya X-baa inafaa katika uchunguzi wa uamilifu wa kishazi elezi katika sentensi changamano za Kiswahili Sanifu?
- iii) Ni kategoria amilifu gani zinazochukuliwa na kishazi elezi katika sentensi changamano?

1.3 NADHARIA TETE

1. Kishazi elezi cha Kiswahili sanifu huweza kuainishwa katika kategoria mbalimbali.
2. Nadharia ya X-baa inaweza kuchanganua kishazi elezi cha Kiswahili kwa uamilifu.
3. Kishazi elezi cha Kiswahili sanifu kina majukumu sawa na ya kirai elezi cha Kiswahili sanifu katika sentensi.
4. Maana ya sentensi haibadiliki tunapobadilisha nafasi ya kishazi elezi katika sentensi.

1.3. SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tumeichagua mada hii kwa kuwa kufikia sasa, hatujapata kuona utafiti uliofanywa kuhusu kishazi elezi cha Kiswahili Sanifu kwa kutumia nadharia ya X–baa.

Kazi nyingi zilizofanywa kuhusu kishazi elezi zinajikita katika sarufi ya Kiingereza. Tulipopitia kazi za wasomi wenzetu tuligundua kuwa kishazi elezi hakijafanyiwa utafiti katika Kiswahili sanifu. Japo sarufi ni sarufi hata ikiwa katika lugha gani, muundo wa kisantaksia wa lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Kiingereza huchukua muundo wa kiima na kiarifu ikiwa uhuru wake wa kubadilisha nafasi za viambajengo vya sentensi ni finyu. Muundo wa Kiswahili wa kiima, yambwa, kiarifu na vitenzi huweza kubadilishwa nafasi katika tungo bila ya kubadilisha maana iliyokuwa hapo awali. Hivi basi mifano katika lugha ya kiingereza huenda ikakosa kukidhi mahitaji yote ya muundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili.

Katika sarufi kiwango cha kisintaksia ndipo uundaji wa sentensi zilizo na maana huchanganuliwa. Vipashio vya sentensi ni neno, kirai na kishazi. Kishazi ndicho kipashio kikubwa katika uundaji wa sentensi. Katika utafiti huu tutashughulikia kiwango cha kishazi. Hii ni kwa sababu kuna umuhimu wa kuweko kwa habari za kishazi elezi katika Kiswahili. Umuhimu huu ni kule kusoma habari unazohitaji kutoka kwa lugha lengwa, badala ya kutafsiri.

Nadharia ya X–baa imetumika sana katika tafiti za Kiswahili zilizofanywa. Kwa kiwango kikubwa nadharia hii imekubaliwa kama nadharia inayoweza kutumika katika uchanganuzi wa lugha ya Kiswahili. Ikumbukwe, nia ya nadharia hii ni kutumika katika ubia wa lugha za kilimwengu.

1.3. UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti wetu utajikita katika Kiswahili sanifu. Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi ambazo zinaweza kushughulikiwa ila hatutazishughulikia lahaja hizo.

Utafiti wetu utajikita katika uchanganuzi wa kishazi elezi pekee. Ni vyema ikumbukwe kuwa kishazi elezi ni aina ya kishazi tegemezi. Kwa hivyo tutavihusisha vishazi vikuu vinavyovibeba vishazi elezi.

Pia kuna nadharia nyingi zingeweza kutumika katika uchanganuzi wa kishazi elezi. Hata hivyo tutajikita katika nadharia ya X- baa kwa mujibu wa nadharia ya Umilikifu na Masharti.

1.6 MSINGI WA NADHARIA


Nadharia tuliyoitumia katika utafiti huu ni nadharia ya X-baa, kwa mujibu wa nadharia ya Umilikifu na Masharti. Nadharia hii inahusu kaida za mpangilio wa viambajengo vya virai. Kwa kuwa kishazi huundwa kwa virai, nadharia hii ilikidhi kwa ukamilifu mahitaji ya utafiti huu. Nadharia hii ya X-baa iliasisiwa na Jackendoff R. na kuendelezwa na Chomsky, N (1957) katika jaribio la kuonyesha miundo ya virai vya lugha. Naye New Meyer (1968:152 – 153) anasema, nadharia ya X-baa ilibadilisha kanuni za miundo virai kwa kutumia ishara hizi:

$$X^{11} - [\text{Kibainishi cha } X^1] X^1$$
$$X^1 - X \dots \dots \dots$$

Muundo wa kishazi kikuu hutofautiana kidogo na kishazi tegemezi. Kishazi kikuu kiulizi kama hiki:

‘Ataweza kupata shahada?’

Lazima kishazi cha aina hii kiwe na kiambajengo cha S-baa. Hivyo basi kitakuwa na muundo ulio sahili. Kama kilivyo kielelezo hapa chini:




Kutokana na mfano huu inatuhitimishia kuwa sio vishazi tegemezi tu vilivyo na muundo wa S- baa. Hata vishazi vikuu viulizi huchukua muundo wa S- baa.

Kufuatana na maendeleo ya kinadharia, vichwa vinanvyosimama bila vibainishi au vijalizo vimechukuliwa kuwa virai kamili. Ouhalia (1991:52) anasema, kutokana na hali hii nafasi hizi huonekana kuwa kapa pale ambapo hazijajazwa kama virai kamili. Kwa

mfano, katika kirai: ‘huyu mtoto mzuri’, kategoria ‘mtoto’ huvurumishwa kwa baa moja kuongezwa kijalizo ‘mzuri’ na kuvurumishwa zaidi katika baa ya pili kwa kuongezwa kibainishi ‘huyu’. Katika mfano huu kichwa cha kirai hiki ni nomino, hivyo basi, kuwa kirai nomino.

* xyz _____




TY

Ouhalia (1991: 52)

Nadharia hii ya X-baa ilitokana na upungufu ulioonekana kuwepo katika nadharia ya sarufi miundo virai. Sarufi miundo virai ilikuwa na kanuni nyingi zilizohusisha kategoria mbalimbali katika uwakilishi wa miundo ya sentensi. Kwa hivyo alitaka kujumuisha kanuni hizi na kuwa kanuni moja. Pia alinua kanuni hii iweze kutosheleza lugha zote za binadamu.

Nadharia ya X-baa ilizuka kama suluhisho la upungufu huu. Nadharia hii ya X-baa inayotumika kuelezea miundo ya virai vya kila lugha ni miongoni mwa nadharia zinazotumika kuunda nadharia ya sarufi bia.

Baada ya Haegeman, L (1991) kutoa mfano wa muundo wa viambajengo katika Kiingereza, aligundua ya kwamba mvurumisho wa skema si huru. Haukuweza kukidhi muundo wa SVO kiima, kitenzi na yambwa (KTY). Yaani haukuweza kutumika katika lugha zote za ulimwengu. Aligundua haya alipochunguza muundo wa Kijapani. Hivyo basi alipendekeza mvurumisho wa skema ufuatao.



v^{II} _____ Spec: v^I


v^{I*} _____ v^I ; xp

v^I _____ v; xp.

Haegman (1991:87)

Haegeman (1991) aliona mvurumisho huu ungeweza kukidhi muundo wa SOV. (Kwamba kitenzi hufuata yambwa na viunganishi), pamoja na muundo wa VO (kitenzi yambwa) pale yambwa inapofuata kitenzi. Hivyo basi mvurumisho huu unaweza kutumika katika lugha bia.

Hebu tutizame skema ifuatavyo:




X inasimamia nomino, kitenzi, kielezi au kihusishi. Sarufi yetu haihitaji kuwa na aina nne za skema, 1. Nomino 2. Kitenzi 3. Kihusishi 4. Kielezi, bali moja tu.

Hivyo basi kielelezo kizima cha muundo wa kirai kimefupishwa na kuwa sheria ya muundo kirai (phrase structure rule) P_s rules. Kategoria ya sarufi inayochunguza miundo ya virai imekuwa maarufu kwa jina la nadharia ya X-baa. Kila kirai kinadhihirishwa na kategoria ya kileksika. Mvurumisho wa kileksika wa kiwango cha juu kabisa ni sarufi X^0 . Nadharia ya X-baa hubainisha mvurumisho wa viwango viwili. Kijalizo huungana na X kujenga mvurumisho wa X^1 ; viunganishi huungana na X^1 kujenga mvurumisho wa X^2 .

Kibainishi huungana na kiwango cha juu kabisa X^1 kujenga mvurumisho wa kiwango cha juu zaidi cha X^{11} . Kwa kawaida twaweza kubadilisha X^{11} na XP) yaani (X^{11} na KX) Katika Kiswahili.

XP	=	KX
ni		ni
X phrase	=	kirai cha X

Kielelezo cha maelezo ya mvurumisho




Sehemu iliyopigwa mstari ndio kirai nomino:

‘Sikutarajia kwamba Wanjiku atatupilia mbali uchunguzi’

T.Y

Haegeman (1991:105)

Hebu tutazame muundo huu wa kirai nomino:



Kile kwa kawaida kilichokuwa kikijulikana kama kiima cha sentensi, hapa ndicho kirai nomino. Ndicho kinachotawaliwa na kirai cha uambishaji kisarufi (U¹¹). Ni vyema tugundue hapa ya kwamba uamilifu wa 'kiima' hautabadilika kwa kuchukua kiima kikiwa peke yake. Katika nadharia ya Umilikifu na Masharti hatuoni agumenti kwa upekee. Uamilifu huu wa agumenti hufafanuliwa katika upangaji umbo la kisintaksia.

Ni vyema pia tufahamu ya kwamba kuna tofauti kati ya mvurumisho wa kirai wa kategoria za kileksika na mvurumisho wa kirai cha uambishaji kisarufi. Kama asemavyo Haegman, (1995) nadharia ya X-baa iliunganisha kanuni zilizokuwepo ndogondogo na kuweza kupata kanuni moja iitwayo kanuni ya skema (Rule schema). Inaweza kudhihirishwa kama ifuatavyo.

$K^{11} \rightarrow$ spesifaya; KK^1 (kikundi husishi)

$P^{11} \rightarrow$ spec; PP^1 (prepositional phrase)

$K^{1*} \rightarrow K^1$; KX

$P^{1*} \rightarrow P^1$; xp

$K^1 \rightarrow K$; KX

$P^1 \rightarrow P$; xp

;-----> yaweza kubadilishwa nafasi

*-----> zaweza kuwa nyingi


UNIVERSITY OF NAIROBI
EASTAFRICANA COLLECTION

Kwamba kila Xp yaani (kX) lazima kiwe na X . X ndicho kichwa cha kirai

Kwa kufanya hivi kategoria zote zimewakilishwa kwa kutumia ishara moja. Hivyo, kuondolea mbali umuhimu wa kategoria. Pia kinyume na nadharia ya sarufi miundo virai nadharia hii inaonyesha uhusiano wa vipengele mbalimbali vya virai.

Mfano wa kishazi elezi kifuatacho:

'Ingawa masomo yalikuwa magumu, tulifuzu'.



Kategoria X hubadilika ili kuwakilisha kategoria zote za kileksika yaani nomino, vitenzi, vivumishi, vihusishi na vielezi. X^{11} ni baa mbili ama uvurumisho wa juu zaidi wa kitengo cha X. X^1 inatoa tafsili ya vijalizo na maana hasa katika vitenzi na vishirikishi. Vijalizo vingi hutokana na nomino, viwakilishi na vivumishi. Chagizo ni aina ya neno ambalo linaweza kujisimamia. Chagizo ni kategoria ambayo hutumika kuelezea vile vipashio vya kielezi ambavyo mara nyingi huwa vielezi na vihusishi. Katika nadharia hii kuna dhana ya kichwa cha kirai ambacho ni ile kategoria inayotawala fungu la maneno.


Kichwa cha kirai kinaweza kuwa mwanzoni ama mwishoni mwa kifungu kinachounda mvurumisho wa X-baa moja kwa kutegemea lugha husika. Kiswahili ni lugha iliyo na nafasi ya kichwa mwanzoni. Vijalizo pamoja na vibainishi ni muhimu katika mvurumisho wa hali ya juu zaidi wa kirai.

Kutokana na mtazamo wa nadharia hii, kirai ndicho kiambajengo muhimu. Kamusi ya Tuki (1990) inasema ‘Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu’. Hapo awali nadharia hii ilitumika katika kuonyesha miundo ya virai pekee vilivyoundwa kutokana na kategoria za kisarufi kama vile: nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na vihusishi, lakini baadaye virai vya kategoria za kiuamilifu kama vile vibainishi, kiima, yambwa, vijalizo na viambishi awali vya uambishaji katika vitenzi vikaingizwa katika nadharia hii, ili kuleta usawazisho wa kimuundo. Kutokana na hali hii vipashio vidogo kama mofu, ambavyo ni viambishi vinavyopachikwa kwenye vitenzi vimeweza kuainishwa katika kategoria hii ya virai. Vipashio vikubwa kama vishazi vimeweza kuchunguzwa kwa kutumia nadharia hii kwani huundwa kwa kuunganisha vipashio vidogo kama vile virai kwa njia ya muungano (Radford 1997: 62) Kutokana na hali hii tumewaza kuchunguza muundo wa kishazi. Mohamed (2001:7) naye anasema kuwa, kwa kijumla kishazi huundwa kutokana na kiima na kiarifu.

Maendeleo haya ya kinadharia yamepelekea kuhusishwa kwa kategoria za kiuamilifu za kijalizo (Kj) ambacho hutangulia vishazi na kitengo cha mnyambuliko (KM) ambacho huambishwa kwenye vitenzi.

Katika nadharia hii muundo wa kishazi umeonekana kuwa wenye viambajengo ambapo (Kj) huchukuliwa na kijalizo cha kitenzi, nomino, vivumishi au kategoria nyingine ilhali ‘S’, ambayo ni kishazi huwa na muundo wa KN na KT. Nafasi ya kirai nomino katika muundo wa kishazi huchukuliwa na kiima cha kishazi. Kielelezo kifuatacho kinadhihirisha muundo wa kishazi.

‘Tunafahamu wazi ‘kuwa Rais ataidhinisha mradi huo’. Nafasi iliyopigwa mstari ni kishazi elezi.



Katika muundo huu KBn 'kuwa' kina uamilifu wa kitenzi kisoukomo. KN ni 'Rais' ambacho kina uamilifu wa kiima na sehemu'ataidhinisha ni kitenzi kilicho na sehemu mbili. Kwanza sehemu ya uambishi 'ata-' na ya pili kitenzi '-idhinisha'. 'Mradi huo' ni kirai nomino. Ikumbukwe kuwa kishazi lazima kiwa na kiima na kiarifu. Sehemu 'ataidhinisha mradi huo', ndio kiarifu cha kishazi. Haegeman (1999 :105) anaeleza ya kuwa kile kinachojulikana kama kiima cha sentensi, hapa ndicho kirai nomino. Kirai nomino hiki ndicho kilichotawaliwa na kirai cha uambishaji kisarufi. Hata hivyo ni vyema tugunduwe ya kwamba uamilifu wa kisarufi wa Kiima hautambuliki kwa kuchukua kiima kikiwa peke yake. Katika nadharia ya Umilikifu na Masharti, hatuoni uamilifu wa agumenti kwa upekee.

1.4. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Polome (1967) anasema kuwa kishazi kinaweza kuwa sentensi kamili inayojitegemea au ikawa ni sehemu ya sentensi. Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha, TUKI (1990) inatueleza kuwa, kishazi ni tungo ambayo ni ndogo yenye uamilifu ndani mwake na inaweza kusimama peke yake au kuwa sehemu ya sentensi.

Crystal (1997:62) anasema, kishazi ni neno linalotumiwa katika baadhi ya mitindo ya kisarufi kumaanisha kipashio katika mpangilio wa kisarufi ambao ni mdogo kuliko sentensi lakini mkubwa kuliko kirai. Mtazamo wa Crystal (1997:62) wa kuwa kishazi ni

kidogo kuliko sentensi hatuafikiani nao. Tukisema kuwa kishazi ni kidogo kuliko sentensi tutakuwa tunamaanisha kuwa sentensi sahili ni ndogo kuliko sentensi.

Jambo hilo halitakuwa sawa. Kishazi tegemezi ndio kidogo kuliko sentensi. Lakini kishazi huru kina dhima sawa na sentensi sahili.

Leech na Svartik (2000: 245) wanasema, kishazi kinaweza kuelezwa kwa njia mbalimbali. Njia mojawapo ni sentensi. Kulingana na uamilifu kuna vishazi huru na vishazi tegemezi. Kategoria ya vishazi tegemezi vimeainishwa kulingana na uamilifu wake katika tungo. Kuna: vishazi rejeshi, vishazi viima, vishazi linganishi, miongoni mwa vingine. Mtazamo wa Leech na Svartik umekita mizizi katika uamilifu. Jambo hili ni tofauti na Crystal. Crystal hakujikita katika ufafanuzi wao. Crystal alifasili kishazi kwa kulinganisha na tungo zingine za kisarufi. Nao Leech na Svartik walizama katika uamilifu bila kuegemea upande wa kulinganisha na kulinganua.

Radford et al (1999: 283) wanasema, kishazi ni utungo wenye kiima na kiarifu na unaweza kuchukua aina ya vipashio vingine kama vijalizo (TY). Kwa mtazamo wetu Radford na wenzake (1999) wamezama katika viambajengo vya kishazi. Hata hivyo ikiwa tutaangalia kuwa utungo wowote ulio na kiima na kiarifu ni kishazi basi tutakuwa tunachanganya na kukanganya fasili ya kishazi na sentensi.

Kwa muhtasari, kishazi hakiwezi kufasiliwa kwa sentensi moja tu bali kwa kujumlisha maoni yote. Kishazi ni kikubwa kuliko kirai na kinatoshana na sentensi sahili au kidogo kuliko sentensi sahili. Kishazi huru ndicho tunachoweza kuchukulia kina dhima sawa na sentensi sahili. Kishazi tegemezi ndicho kilicho kidogo kuliko sentensi sahili. Ni utungo

ulio na kiima na kiarifu. Kishazi kina uamilifu wake katika sentensi. Leech na Starvik (2000) wanaainisha na kufasili vishazi kwa misingi ya uamilifu wake.

Hapa ndipo tunapata aina ya vishazi. Tofauti kubwa inayojitokeza hapa ni kuwa, kitenzi peke yake chaweza kujisimamia kama sentensi. Lakini kishazi lazima kiwe na kiima na kiarifu.

Householder (1972) anasema vishazi katika sentensi vinajulikana wazi kuwa hutofautiana sana katika kuwa huru na kujitegemea katika uhusiano baina yao. Tofauti hizi ziko kati ya uambatani na utegemezi. Maelezo kamili juu ya tofauti hizi.

Syntactic Theory I Structuralist, Householder (1972) anasema, vishazi katika sentensi vinajulikana wazi kuwa hutofautiana sana katika kuwa huru au kujitegemea katika uhusiano baina yake. Tofauti hizi ziko kiwango kati ya uambatani na utegemezi. Maelezo kamili juu ya tofauti hizi:

Masiala haya yanaweza kugawanyika kama ifuatavyo

1. Ni katika fasili gani kuwa kishazi tegemezi ni kishazi?
2. Twawezaje kutofautisha na kutambua aina zingine za vishazi kama vile tegemezi, kikuu na ambatani?
3. Je huenda ikawa kuna aina zingine zaidi ya vishazi kando na kishazi tegemezi?

Majaribio yamefanywa ili kuweza kutoa maelezo ya utegemezi kama umbo, maana na uamilifu wake. Kwa hivyo maelezo haya yatazingatia dhana na mitazamo tofauti ifuatayo: Kwanza kimofolojia, pili kisemantiki na tatu kisintaksia au kimantiki.

Mtazamo wa kimofolojia:

Kishazi tegemezi hujulikana kutokana na umbo lake, yaani kuweko kwa maneno fulani kama vile maneno husishi. Maneno husishi haya ni kama vile: kiwakilishi nomino na viunganishi, uhusika na dhamira.

Curme, kama alivyonukuliwa na Householder (1972:23) anatofutisha kuwa: kuna kishazi kiima, kiarifu, kivumshi, yambwa na kishazi elezi. Alimalizia kwa kueleza kuwa, ni vyema tufahamu umuhimu wa vishazi katika lugha ya binadamu.

Mtazamo wa Kisemantiki:

Katika mtazamo huu, wanaona kuwa shida iliyo kuhusu umbo huathiriwa na fahiwa. Kuna pendekezo limetolewa la kuweza kutofautisha kati ya uambatani na utegemezi. Kisemantiki na kiwango kingine katika uhusiano na umuhimu wa kisaikolojia, kisemantiki huleta maana kimuktadha, na kishazi kikuu huleta maana kwa kutengwa kikiwa peke yake (in isolation). Japo lazima tukumbuke sio rahisi kishazi kutengwa kabisa na kuwa peke yake, lazima kishazi kile kihusishwe kimuktadha au kihali.

Mtazamo wa Kimantiki:

Kishazi tegemezi kinaweza fasiliwa kama kinachotegemewa, au kinachoelekeza au kinachofaulisha.

Mtazamo wa Kisintaksia:

Mtazamo wa Kisintaksia ndio mtazamo utakaoegemewa na utafiti huu. Householder akimnukuu Girad (1747) anaeleza kuwa, kishazi tegemezi ni wasilisho la utungo wa sentensi. Jespersen (1924, 1933:166) ameeleza kishazi tegemezi kama, “Mojawapo ya sentensi iliyo na umbo sawa na lile la sentensi”.

1. Kwa kutumia matamshi yaliyotamkwa peke yake tunaweza kufahamu maneno yaliyotegemeana, yanayojisimamia na yaliyogawanyika kinasibu.
2. Hapa kwa kutumia ufafanuzi mwingine, kishazi kinafafanuliwa kuwa ni tungo kamili ya kisintaksia. Hii ni kumaanisha kuwa hujisimamia peke yake. Mtazamo wa kisintaksia unamaanisha tungo hiyo haina majukumu yoyote ya kisintaksia katika matamshi.
3. Kishazi msingi: hiki ni kishazi chochote kile kisichokuwa na uamilifu wowote wa kisintaksia wala uamilifu wowote ndani ya kishazi kingine. Chenyewe chaweza kujiambia matamshi yasiyo ya kisintaksia.
4. Mfano wa vishazi msingi:
 - (i) Ni mgonjwa.
 - (ii) Yeye ni mgonjwa? Ndio.
 - (iii) Analala kitandani – Yu kitandani?! Kwa sababu yu mgonjwa.

Katika kazi yao, Quirk na Greenbaum (1973) wameainisha vishazi huru na vishazi tegemezi na kuvichanganua.

Zaidi ya hayo wametoa uchanganuzi wa kina wa vishazi elezi na kutoa mifano mwafaka katika lugha ya kiingereza. Kazi hii ya Quirk na Greenbaum (1973) ndio iliyokuwa msingi wa utafiti huu.

Vitale (1981) amechanganua sentensi za Kiswahili katika *Swahili Syntax*. Ameshughulikia kishazi kwamba kwa kina. Uchanganuzi na mifano yake imetusaidia kuelewa zaidi juu ya kishazi.

Kazi ya Massamba na wenzake (1999) ni jaribio la kuchanganua sentensi za Kiswahili na vipashio vyake kwa kina. Kazi hii inashughulikia vipashio vinavyounda sentensi. Kazi mojawapo ikiwa ni kishazi. Katika kazi hii, wataalamu hawa wanaviainisha vishazi vya Kiswahili na kutoa mifano kwa kila aina ya kishazi. Kazi hii imetufaidi sana katika kutupa mwelekeo na msingi wa uanishaji wa vishazi vya Kiswahili Sanifu.

Katika kazi yake ya *Modern Swahili Grammar*, Mohammed (2001) ameshughulikia vishazi vya Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake. Aliainisha vishazi vya Kiswahili kama: vishazi vikuu na vishazi tegemezi vya Kiswahili. Alipiga hatua zaidi na kuviainisha vishazi tegemezi.

Katika tasnifu yake ya M.A. Jerono (2005) alichanganua kishazi arifu cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa ambayo ni mojawapo ya nadharia ya Umilikifu na

Masharti. Kazi yake ilituungazia matumizi ya nadharia hii katika uchanguzi wa kishazi huru cha Kiswahili.

Kazi hii itatupa mwanga kuhusu muundo wa kishazi huru cha Kiswahili. Kishazi huru ambacho ni muhimu katika utafiti huu tutakitumia katika uchanganuzi wa kishazi elezi pia.

Katika tasnifu yake ya M.A, Swaleh (2005) amechunguza kishazi cha kitikuu. Kitukuu ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili. Kazi hii nayo pia imetupa msingi wa uchanganuzi wa kishazi hasa kwa kutumia mtazamo wa uminimalisti.

Katika tasnifu yake ya M.A, Mutua (2005) ameshughulikia kishazi tegemezi cha Kiswahili Sanifu kwa mtazamo wa X-baa. Kazi hii itatuelekeza katika uainishaji wa vishazi na jinsi vinavyohusiana kimofosintaksia.

Hitimisho kuhusu vishazi:

twaweza kuhitimisha kwa kutumia mambo manne makuu:

- i. Kishazi kilichoning'inizwa kilicho na kijalizo cha utoano ni kiambajengo cha S- baa.
- ii. Kishazi kilichoegemezwa ambacho hakina kijalizo cha utoano pia kina muundo wa S-baa (kikiwa na KBn)
- iii. Vishazi vikuu vilivyo na kijalizo cha utoano au kitenzi kisaidizi ni viambajengo vya S- baa.

- iv. Vishazi vikuu visivyokuwa na kijalizo cha utoano au kitenzi kisaidizi ni viambajengo vya S-baa (havina KBn)

1.5. MBINU ZA UTAFITI

Tumefanya utafiti huu kwa kudurusu vitabu na majarida mbalimbali. Tumepitia vitabu na tasnifu zilizo na fasili pamoja na matumizi ya nadharia tuliyotumia. Vitabu hivi viliweza kutuendeleza zaidi na kufahamu jinsi ya kuitumia nadharia hii katika utafiti wetu. Pia tulisoma kazi mbalimbali za utafiti ili kuhakikisha kuwa tumepata mawazo ya wasomi wengine ndipo tuweze kuyalinganisha na kuyalinganua na mawazo na matokeo ya utafiti wetu.

Kwa kuwa mtafiti ana ujuzi wa lugha ya Kiswahili, alitumia ujuzi wa lugha hii kuzalisha data. Mtafiti pia alitumia ujuzi wa wasomi wenzake kupata data zaidi ili kuchanganya mawazo tofauti katika kazi hii. Ili kuweza kutambua kategoria za kileksika na agumenti, tulichanganua data kwa kutumia nadharia ya X-baa. Tulibadilisha nafasi za vishazi elezi katika tungo, ili kuweza kuchunguza kama maana hubadilika kishazi elezi kinapobadilishwa nafasi katika senten

Mtafiti si mzungumzaji mzaliwa wa Kiswahili sanifu. Kwa hivyo baada ya kuzalisha data yake, alitumia wazawa wa Kiswahili pamoja na maguru wa Kiswahili sanifu kumsaidia kuchanganua na kuhakiki muundo, usanifu na ukweli wa data aliyokusudia kutumia katika utafiti huu.

SURA YA PILI

KISHAZI ELEZI CHA KISWAHILI SANIFU

UTANGULIZI

Tunatarajia baada ya kuchanganua kishazi elezi, tutajaribu kutazama maelezo ya wanaisimu wote tuliorejelea juu ya dhana ‘kishazi’ kama yana mashiko. Tunatarajia kupata kina zaidi cha dhana hii ya kishazi kabla ya kuchanganua kishazi elezi. Katika sura hii tutaviainisha vishazi elezi na kuvifafanua. Baadaye tutatoa mifano katika kila aina ya kishazi ambacho kimeainishwa. Katika kila mfano tutaeleza uamilifu wa kishazi husika.

2.1 DHANA YA VISHAZI

Ufafanuzi wa dhana ya kishazi una mwingiliano mkubwa sana wa dhana ya sentensi sahili. Hii ni kwa sababu wanaisimu wengi huvipa vipasho hivi hadhi tofauti katika sintaksia.

Kimundo kishazi ni kipasho ambacho kina kiima na kiarifu. Tukumbuke maelezo haya hutumiwa pia kueleza sentensi sahihi. Crystal, (2000:72) katika kubainisha tofauti iliyo kati ya sentensi sahili na kishazi kihadhi, anaeleza kuwa, kishazi ni dhana inayotumiwa kurejelea kipashio cha kisarufi, ambacho ni kidogo kuliko sentensi lakini kikubwa kuliko kirai, maneno na mofimu. Swali ni: ni nini haswa kipimo cha ukubwa na udogo huu?

Huddleston, (1984) anatupa maelezo zaidi kwa kusema kuwa, mpaka baina ya sentensi na kishazi huingiliana, iwapo kishazi kitajisimamia (yaani sentensi sahili) bila kutumiwa kama kiambajengo cha sentensi na kupoteza hadhi hii kinapotumiwa katika sentensi nyingine. Ukubwa na udogo unaozungumziwa hapa tutauchukulia ni kule kuwa na kiima na kiarifu au kutokuwa na kiima na kiarifu mtawalia. Katika utafiti huu, kipande kitachokuwa na kiima na kiarifu ndicho tutachukulia kuwa ni kishazi.

Wazo hili linajitokeza vyema katika mfano ufuatao;

- Kanjeri ni mtoto mzuri.
- Ingawa kanjeri ni mtoto mzuri, ataolewa na Ali.
- Ingawa kanjeri ni mtoto mzuri anayependwa na wengi, ataolewa na Ali.

Sehemu iliyopigwa mstari ni kishazi elezi cha “hali”, kinaelezea Kanjeri ni mtoto wa aina gani.

Wanasarufi mapokeo waliainisha vishazi katika makundi mawili makuu:

- i. Vishazi huru
- ii. Vishazi tegemezi

Vishazi huru ni vishazi ambavyo hujitosheleza kimaana. Kwa mfano:

‘Aliimba vizuri’.

Vishazi tegemezi haviwezi kujitosheleza bila ya kushirikiana na vishazi vingine. Huwa havina maana vikiwa peke yake.

Maelezo ya wanamofolojia, wanasintaksia na wanasemantiki wanatofautiana. Polome (1967:156) kama mwanamofolojia anadai kuwa, “*Kishazi* kinaweza kuwa sentensi katika ukamilifu wake au sehemu ya sentensi. Kina... kiima na kiarifu”. Japokuwa Polome ni mwanamofolojia anatumia istilahi za Kisintaksia: ‘kiima’ na ‘kiarifu’. Istilahi hizi katika sintaksia hutumika kueleza uamilifu wa viambajengo katika tungo. Dai la Polome kuwa sentensi inaweza kuwa kishazi au kishazi kuwa sehemu ya sentensi lina mashiko.

Householder, (1972) na Brondal, (1972:27) wanaeleza kuwa, “Kishazi ni...utungo wa Kisintaksia uliokamilika,... ule ambao una uhuru wake katika mtazamo wa Kisintaksia. Utungo huu hauna dhima yoyote katika matamshi”. Kutokana na madai ya Brondal, vishazi ili viwe vishazi lazima viwe vimekamilika Kisintaksia au vina uhuru Kisintaksia. Ili utungo uwe na uhuru wake Kisintaksia lazima ubebe wazo au ujumbe uliokamilika. Hivyo ni Kumaanisha utungo huo uwe na kiima na kiarifu. Hata kama Brondal hajatumia dhana hizi ‘kiima’ na ‘kiarifu’ ni muhimu katika utafiti huu. Swali ni kuwa, mbona tena kuna vishazi tegemezi? Kwa mujibu wa Brondal, ili kishazi kiwe kishazi, lazima kiwe na ukamilifu wake. Yaani kibebe ujumbe uliokamilika.

Quirk na wenzake, (1973:310) wanadai kuwa “vishazi...kila wakati vina kiima na kiarifu...”. Maelezo yao yanaeleza zaidi kuwa inategemea ‘muundo wa utungo’. Iwapo ni sentensi ya kuamrisha au dondoshi viima huwa havipo. Katika kuainisha kwao kwa vishazi tunakumbana na vishazi viso na vitenzi. Iwapo vitenzi ndivyo vichwa vya virai tenzi ambavyo ndivyo viarifu, swali ni: Je, kutakuwaje na vishazi viso na vitenzi?

TUKI, (1990:12) inaeleza kuwa, “Kishazi ni tungo ambayo ni ndogo yenye uanifu ndani mwake. Jambo linaloleta utata ni ‘ndogo’. Ndogo kiasi gani? Au udogo huu utapimwa na kipimo gani? Neno, kirai na hata sentensi ni tungo zinazoweza kuwa ndogo zenye uanifu ndani mwao. Je, iwapo tungo yoyote ni ndogo yenye uanifu ndani mwake itakuwa ni kishazi?”

Radford na wenzake, (1999:283) wanadai kuwa, “Kishazi ni utungo wenye kiima na kiarifu na unaweza kuchukua vipashio vingine kama vijalizo.” (TY). Kutokana na maelezo haya tunaafikiana kuwa utungo wowote ulio na kiima na kiarifu ni kishazi. Wanaongeza kuwa utungo huu: ‘kishazi’ unaweza kuchukua vipashio vingine. Je, ni kweli vishazi vinaweza kuchukua vipashio vingine?”

Leech na Svartvik, (2000:245) wanaeleza kuwa, “Kishazi kinaweza kuelezwa kwa njia mbalimbali. Njia mojawapo ni kulingana na uamilifu wake. Yaani uamilifu wa kishazi katika sentensi. Kutokana na uamilifu kuna vishazi vikuu na vishazi tegemezi.” (TY). Kutokana na ufahamu wetu Leech na Svartvik ingawa wanafafanua vishazi katika misingi ya uamilifu wanaonelea kishazi kuwa ni sehemu ya sentensi. Hii ni kwa sababu wanatazama uamilifu wa kishazi katika sentensi.

Crystal, (2003:74) anaeleza kuwa, ‘Kishazi ni istilahi itumiwayo katika maelezo mbalimbali kurejelea kipashio cha kisarufi kilicho kidogo kuliko sentensi lakini kikubwa kuliko kirai, neno au mofimu’”. (TY) Mawazo ya Crystal yanafungamana na ya Leech, Svartvik pamoja na Radford, kuwa vishazi ni vidogo au ni sehemu ya sentensi.

TUKI (2004:36) inaeleza kuwa, “kishazi ni tungo yenye kiima na kiarifu ambayo imo ndani ya tungo kuu”. Kunajitokeza utata katika maelezo haya. Je, tungo kuu inayozungumziwa hapa ni sentensi, kirai au ni neno? Ingalikuwa vyema zaidi kama kamusi hii ingalifafanua maelezo haya zaidi. Hata hivyo inaonelea kishazi kuwa na kiima na kiarifu. Maoni haya yanaungana na ya Brondal, (1972) na Quirk na wenzake, (1973).

Mwalili, (2008:47) akimnukuu Huddleston, (1984) anaeleza kuwa, “Mpaka baina ya kishazi na sentensi huingiliana iwapo kishazi kitaweza kujitegemea chenyewe (yaani sentensi sahili) bila kutumiwa kama kiambajengo cha sentensi na kupoteza hadhi kinapotumiwa katika sentensi nyingine”.

Baada ya kuchunguza fafanuzi mbalimbali kuhusu vishazi kwa mujibu wa wasomi hawa, tutakubaliana fafanuzi hizi zinaegemea misingi miwili. Msingi wa kimofolojia (umbo) na wa Kisintaksia (uamilifu). Msingi wa umbo unalinganisha kishazi na sentensi, kirai, neno na mofimu. Katika msingi huu udogo au ukubwa wa kishazi hufananishwa na viambajengo vya utungo. Uamilifu nao ni wa kiima na kiarifu, istilahi ambazo ni za kisintaksia. Brondal (1972), Polome (1967), Quirk na wenzake, (1973), Radford, (1999), TUKI (2004), wanaegemea kwenye msingi huu wa uamilifu. Kwa maoni yetu, misingi hii miwili ni muhimu na inakamilishana.

Katika utafiti huu tutafafanua kishazi kama utungo wa kisintaksia au kisarufi wenye umbo sawa na wa sentensi sahili, ulio na kiima na kiarifu. Vishazi viso na vitenzi, dondoshi na vya kuamrisha, katika umilisi wa mzungumzaji mzaliwa wa lugha ya

Kiswahili Sanifu au lugha yoyote ile husika anafahamu kuwa vipo, hata kama katika umbo halisi, sehemu hizi: kiima au kiarifu hazionekani.

2.2 AINA YA VISHAZI ELEZI

Katika Uchanganuzi wetu tutatumia kishazi elezi katika nafasi tatu katika sentensi. Hii itatusaidia kuchunguza kama kishazi elezi husika kitaweza kustiri uamilifu wake. Pia kama kishazi elezi kile kitabadilisha maana ama kuipoteza maana katika sentensi husika. Sehemu kishazi elezi kitakapojitokeza ni:

- i. Mwanzoni mwa sentensi.
- ii. Mwishoni mwa sentensi na
- iii. Katikati ya kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu/katikati mwa kiima na kiarifu.

Baada ya kupitia kazi za: Quirk R. na Greenbaum (1973), Mittins, W.H (1962), Householder, F.W (1972), Polome, E (1967), Jerono, P (2005) na Mwalili, M. N, (2008), tuliweza kuainisha vishazi elezi kama ifuatavyo:

Sehemu zilizopigwa mstari katika kila sentensi ndizo sehemu zinazowakilisha kishazi elezi.

2.2.1 Kishazi elezi cha wakati.

Kishazi elezi cha wakati hutangulizwa na vitegemezi kama, baada ya, kabla, tangu, mpaka na kadhalika.

(ia) Tangu tulipotoka Nairobi, mvua imenysha sana.

Katika sentensi hii kishazi kikidondolewa kutabaki na ‘mvua imenysha sana’. Msikilizaji yeyote atakayeambiwa ‘mvua imenysha sana’ bila kuwa na mazungumzo yoyote hapo awali, atauliza maswali kama; Lini? Kwa hivyo? Saa ngapi? Kweli? na kadhalika. Kumaanisha ya kuwa ujumbe utakuwa bado haujakamilika. Pale kishazi elezi kinapongezewa ujumbe utakamilika.

Tukibadilisha nafasi ya kishazi elezi kije mwisho wa sentensi, kama hivi:

(ib) Mvua imenysha sana tangu tulopotoka Nairobi.

Maana inabaki ileile ya kwanza. Kuwa mvua imekuwa ikinyesha sana tangu watoke Nairobi, japo msisitizo unasikika kuwa uko katika mvua kunyesha wala sio wakati kama vile kishazi kinapokuwa katika sehemu ya kwanza ya sentensi.

(ic) Mvua, tangu tulipotoka Nairobi imenyeshwa sana.

Ujumbe umebaki uleule. Sentensi inasikika kama jibu la swali fulani. Mkazo u katika mvua kunyesha. Sentensi (ia), (ib) na (ic) tunapata ujumbe mmoja kwa ujumla. Ujumbe ni kuwa mvua imekuwa ikinyesha, wakati mvua hii imekuwa ikinyesha ni tangu walipotoka Nairobi.

Hii inamaanisha ya kuwa katika kishazi elezi cha wakati kinapobadilishwa nafasi zake katika sentensi sehemu ya kusisitizwa ndiyo hubadilika na wala sio ujumbe kwa ujumla.

(iia) Baada ya Kenya kunyakua uongozi kutoka kwa mbeberu, ufisadi ulianza kuota mizizi.

Sentensi hii msisitizo u katika wakati. Ni wakati gani haswa ufisadi huu ulipoanza kuota mizizi. Mzungumzaji anaona ya kuwa labda kama uongozi ungalibakia kwa mbeberu ufisadi haungalikuwepo. Kwa kuwa tangu mkenya aliponyakua uhuru wake, basi ufisadi ndipo ulipoota mizizi.

(iib) Ufisadi ulianza kuota mizizi baada ya Kenya kunyakua uongozi kutoka kwa mbeberu.

Hapa sentensi inaeleza ufisadi ulianza kuota mizizi lini? Hapa mzungumzaji analalamikia hali ya ufisadi huu. Msisitizo u katika ufisadi.

*xyz_____

(iic) Ufisadi baada ya Kenya kunyakua uongozi kutoka kwa mbeberu ulianza kuota mizizi.

Hapa inaeleweka wazi kuwa ufisadi uko. Unaeleweka pia ulianzaje na wala hakuna malalamiko yoyote mzungumzaji aliyonayo.

(iiia) Tulifika mjini mwendo wa saa tano asubuhi mvua ilipoanza kunyesha kabla ya harakati kuanza.

Mzungumzaji anajulisha wakati walipofika mjini.

(iiib) Mwendo wa saa tano asubuhi mvua ilipoanza kunyesha kabla ya harakati kuanza, tulifika mjini.

Hapa sentensi inaelezea kilichofanyika wakati uliotajwa. Kilichofanyika ni kuwa walifika mjini. Hii ni kinyume na sentensi (iiia) inayoeleza wakati waliofika mjini.

*xyz_____

Tulifika mwendo wa saa tano asubuhi mvua ilipoanza kunyesha kabla ya harakati kuanza mjini.

Sentensi hapa imepoteza maana.

2.2.2 Kishazi elezi cha mahali

Kishazi elezi cha mahali hutangulizwa na kiwakilishi cha mahali kwa mfano; popote, momote au kokote. Mifano katika sentensi:

(ia) Wasomi wa Kenya huenda kokote wanakohitajika na kuthaminiwa.

Sentensi hii inaeleza kuwa wasomi hawa hakuna mahali wanaweza kukosa kwenda. Mradi tu mahali hapo watathaminiwa. Thamani hii bila shaka ni ya ujuzi walio nao.

(ib) Kokote wanakohitajika na kuthaminiwa, wasomi wa Kenya huenda.

Sentensi hii ina msisitizo wa mahali wasomi wa Kenya huenda. Kule wanakohitajika na kuthaminiwa ndiko wasomi hawa huenda.

(ic) Wasomi wa Kenya kokote wanakohitajika na kuthaminiwa huenda.

Sentensi hii nayo inataka kutujulisha wafanyavyo wasomi wa Kenya. Wasomi wa Kenya kokote wanakohitajika na kuthaminiwa wao huenda.

(ia) Pahali jumba lilipochomeka, hatukuona chochote ila jivu.

Sentensi hii inazungumzia mahali mahususi pale jumba lilipochomekea. Katika mtazamo wa kimfosintaksia kuna upatanisho wa ngeli katika tungo nzima.

(iib) Hatukuona chochote ila jivu Pahali jumba lilipochomeka.

Mkazo u nominoni. Kuwa hakuna chochote kilichobakishwa na moto. Mzungumzaji anataka kuonyesha jinsi moto huo ulivyoteketeza jumba hilo.

(iic) Hatukuona chochote Pahali jumba lilipochomeka ila jivu.

Hapa napo msisitizo u katika kutoona kitu (yaani mabaki ya nyumba) kilichoonekana ni jivu.

Katika mtazamo wa kimfosintaksia kuna upatanisho wa ngeli katika tungo nzima. Hebu tuchunguze na kuchanganua tungo zifuatazo.

(ia) kokote wanakothaminiwa

(iia) pahali jumba lilipochomeka.

Katika sentensi ya (ia) kuna upatanisho wa ngeli ya *Ku* na katika sentensi (iia) upatanisho wa *Pa*. Upatanisho huo unapokosekana sentensi au tungo huleta mushkil. Kwa mfano, badala ya utungo ulioko (ia) tuwe na:

Kokote wanapothaminiwa.

Mofimu *ko* na *po* hazina upatanisho wa kimofosintaksia zinapotumika pamoja. Mofimu *ko* na *po* zi katika ngeli tofauti za mahali. Mofimu *ko* ni ya ngeli ya KU {mahali jumla}. Mofimu *po* ni ya ngeli ya PA. {mahali mahususi}. Kwa hivyo, maana ya tungo hii itakuwa na utata. Wasomi hawa hawaendi mahali mahususi panapojulikana bali huenda kokote. Ngeli ya {mahali jumla} ndio mwafaka kutumika katika maana iliyokusudiwa.

2.2.3 Kishazi elezi cha masharti na ukubalifu

Kishazi elezi cha masharti na ukubalifu hudhihirisha utegemeaji wa hali moja au seti ya hali kwa nyingine. Kishazi elezi cha ukubalifu nacho hutangulizwa na kiunganishi ‘ingawa’. Mifano ni kama ifuatavyo:

(ia) Ingawa maisha yana changamoto zake, lazima tukabiliane nayo.

Sentensi hii ina sharti kuwa lazima tukubaliane na changamoto za maisha. Ukubalifu ulioko ni kuwa, maisha yako na yana changamoto zake.

*xyz_____

(ib) Lazima tukabiliane nayo Ingawa maisha yana changamoto zake.

Ukubalifu ulioko ni kuwa maisha yako na lazima tukubaliane na maisha yalivyo. Sentensi hii haisisitizi kule kuwepo kwa changamoto za maisha. Kinachokubaliwa hapa ni maisha na wala sio changamoto zake.

*xyz_____

(ic) Lazima Ingawa maisha yana changamoto zake tukabiliane nayo.

Hakuna budi iliyoko hapa ni ya kukubali maisha pamoja na changamoto zake. Sharti lililopo ni kuwa maisha yana changamoto zake. Hatuna budi kukubaliana na haya maisha kwani tuko maishani tayari.

(iia) Kama mgomo wa waalimu hautafutiliwa mbali na chama cha walimu, hakutakuwa na masomo shuleni.

Katika sentensi hii kuna upatanifu wa masharti na ukubalifu. Kwamba mgomo ni wa waalimu. Unaongozwa na chama cha waalimu. Kwa vile kuna mgomo hakuna masomo yanayoendelea. Mgomo unaweza kufutiliwa mbali. Lakini mgomo huu unaweza kufutiliwa mbali na chama cha waalimu. Masharti yaliyoko hapa ni kuwa, masomo kuwepo lazima mgomo uwe umefutiliwa mbali. Ukubalifu uliopo ni kwamba, hakuna anayeweza kufutilia mbali mgomo huu, isipokuwa chama cha waalimu. Pia, mgomo wa walimu umeathiri masomo shuleni. Kwa hivyo mgomo ndio uliosababisha kutokuwepo na masomo shuleni.

(iib) Hakutakuwa na masomo shuleni kama mgomo wa walimu hautafutiliwa mbali na chama cha walimu.

Mkazo u katika masomo. Masomo hayatakuweko kama mgomo wa walimu hautafutiliwa mbali. Ukubalifu uliopo ni kuwa masomo hayatakuwepo kwa kuwa kuna mgomo wa walimu.

*xyz_____

(iic) Hakutakuwa na masomo kama mgomo wa walimu hautafutiliwa mbali na chama cha walimu shuleni.

Hapa inamaanisha kuwa mgomo huu unafanyikia shuleni na wala sio masomo yaliyo shuleni. Tunagundua katika vishazi hivi vya masharti na ukubalifu maana inaweza kubadilika pale kishazi kinapobadilishwa nafasi yake katika sentensi. Japo ujumbe utakao kuwa unajitokeza ni wa kijumla.

2.2.4 Kishazi elezi cha sababu

Kishazi elezi cha sababu hutangulizwa na viunganishi vitegemezi kama vile; kwa sababu, kwa vile na vinginevyo.

Mifano ni kama ifuatavyo:

(ia) Nilimkopesha pesa kwa sababu alizihitaji.

Katika sentensi hii ya kwanza kishazi kinaeleza sababu ya kitendo cha kukopesha pesa. Sababu ni kuwa alizihitaji. Kukopeshwa pesa ndiko kulikoleta mazungumzo. Sentensi hii inaangazia kukopesha pesa zaidi kuliko uhitaji aliokuwa nao.

(ib) Kwa sababu alizihitaji nilimkopesha pesa.

Katika sentensi hii nayo kinachoangaziwa zaidi ni uhitaji aliokuwa nao. Uhitaji huu ulifanya akopeshwe pesa. Ujumbe kwa ujumla unabakia uleule, kinachobadilika ni msisitizo wa kinachoangaziwa zaidi.

*xyz_____

(ic) Nilimkopesha kwa sababu alizihitaji pesa.

Hapa kinachosisitizwa ni kule kupewa pesa. Kama si kuhitaji pesa hizo hangalikopeshwa.

(iia) Kwa vile Yusufu alipendwa zaidi na wazazi wake, ilitibi ahujumiwe na ndugu zake.

Kishazi elezi kinaeleza sababu ya Yusufu kuhujumiwa na nduguze. Sababu yenyewe ni kuwa, Yusufu alipendwa na wazazi wake zaidi.

(iib) Ilibidi ahujumiwe na ndugu zake kwa vile Yusufu alipendwa zaidi na wazazi wake.

Maana inabakia ileile hapa. Jambo linaloangaziwa zaidi hapa ni kuhujumiwa. Tunapewa sababu za kuhujumiwa kinyume na 'ia' inavyotuelezea matokeo ya kupendwa zaidi kwa Yusufu.

*xyz_____

(iic) Ilibidi kwa vile Yusufu alipendwa zaidi na wazazi wake ahujumiwe na ndugu zake.

Msisitizo zaidi uko katika ile hali ya kutokuwa na uchaguzi. Japo maana ya kijumla tunaipata ilivyokuwa imekusudiwa awali. Japo muundo wa sarufi ni hafifu. Kitenzi kisaidizi kwa kawaida hufuatana na kitenzi kikuu. Hapa kimefuatana na kishazi elezi.

2.2.5 Kishazi elezi cha hali

Kuna wakati kishazi elezi cha hali hutangulizwa na Kibainishi 'kuwa'. Kwa mfano:

(ia) Tulifunga safari tulipoona kuwa hali ya anga ilikuwa shwari.

Sentensi hii kishazi kinazungumzia hali ya anga. Hali yenyewe ilikuwa shwari. Kinaelezea hali ilivyokuwa wakati safari hii ilipofungwa. Katika mpangilio wa maneno tunagundua ya kwamba kitenzi kinatangulia nomino.

(ib) Tulipoona kuwa hali ya anga ilikuwa shwari tulifunga safari.

Kinachoangaziwa zaidi hapa ni ile hali ya anga ilivyokuwa. Hii ni kinyume na sentensi (ia) inayoangazia kule kufungwa kwa safari. Maana ya kijumla inapatikana.

*xyz _____

(ic) Tulifunga tulipoona kuwa hali ya anga ilikuwa shwari safari.

Huu sio muundo sahihi. Kishazi hiki kinapojitokeza katikati mwa sentensi maana hupotea. Sentensi hubaki na maana inayoeleweka kijumla.

Hebu tutazame kishazi elezi cha hali kingine kilicho na kibainishi 'kuwa'. Je, nacho pia kitakuwa na matokeo yaliyoko (ic)

(iia) Ilinibidi kusafiri kwa ndege kwa kuwa barabara haikuweza kupitika.

Hali ya barabara ndiyo inayozungumziwa hapa. Hali ya barabra ndiyo iliyosababisha kitendo cha kusafiria ndege.

Hebu tutangulize kitenzi kisaidizi.

(iib1) Kwa kuwa barabara haikuweza kupitika ilinibidi kusafiri kwa ndege.

Huu ndio mpangilio wa kawaida wa maneno katika Kiswahili sanifu. Maana ni ileile inayopatikana katika (iia).

(iib2) Kwa kuwa barabara haikuweza kupitika, kusafiri kwa ndege ilinibidi.

Hatuzungumzi hivi katika hali ya kawaida. Japo maana inayowakilishwa inapatikana bila ugumu wowote. Hebu tudondoe kitenzi kisaidizi:

*xyz_____

(iib3) Kwa kuwa barabara haikuweza kupitika kusafiri kwa ndege.

Tunagundua hapa kuwa utungo huu haujakamilika kuwa sentensi. Hauna mantiki. Haijulikani kusafiri kwa ndege huku ni kwa kila mtu, ni kwa mzungumzaji, kutayarishwe au ndiyo suluhisho?

Hatuwezi kuhitimisha kwa kusema matokeo ya kitenzi kisaidizi kinapodondoshwa au kinapotanguliwa na kitenzi kikuu, Haswa pale kishazi elezi cha hali kinapokuwa katika sehemu ya kwanza katika sentensi. Data kubwa itahitajika kukamilisha hoja hii.

*xyz_____

(iic) Ilinibidi kwa kuwa barabara haikuweza kupitika kusafiri kwa ndege.

Kitenzi kisaidizi ndicho kilichochukuwa sehemu ya kwanza ya sentensi. Kwa kawaida sivyo tunavyozungumza. Japo maana na ujumbe wa sentensi hii unapatikana na kueleweka, mzungumzaji alisafiri kwa kutumia ndege. Kitendo hiki kilisababishwa na hali ya barabara ilivyokuwa.

Wakati mwingine kishazi elezi cha hali hukosa kuwa na kitangulizi. Kwa mfano:

(iiia) Raila alikubali kugawa mamlaka, hali ya wasiwasi ilipozidi.

Sentensi hii inatufafanulia hali iliyosababisha Raila kukubali kugawa mamlaka. Hali ya sintofahamu ilikuwa imezidi kunoga. Kitendo cha ‘kukubali’ kimetokana na hali ilivyokuwa mbaya.

(iiib) Hali ya wasiwasi ilipozidi, Raila alikubali kugawa mamlaka.

Sentensi ya pili nayo inatufafanulia hali iliyosababisha Raila kukubali. Hali ilikuwa ya ‘wasiwasi’. Uzuri wake alikubali. Kitendo cha ‘kukubali’ kimetokana na hali ilivyokuwa, hali ya kutojulikana ni lipi lingine lingalitokea? Sentensi hii maana imebakia ileile bila kubadilishwa msisitizo wake.

(iiic) Raila, hali ya wasiwasi ilipozidi, alikubali kugawa mamlaka.

Kishazi kinapotokea katikati ya kiima na kiarifu, maana na msisitizo wa sentensi hii unabakia uleule. Japo vishazi aina hii (tegemezi) vinatakiwa kutanguliwa na viunganishi vitegemezi, ndipo viweze kuchukua lile umbo la utegemezi, kishazi hiki tunagundua ya kuwa hakina kiunganishi kitegemezi. Ijapokuwa kishazi hiki hakina kiunganishi kitegemezi kishazi hiki hakijitegemei. 'hali ya wasiwasi ilipozidi', utungo huu haujakamilika. Hatujaarifiwa hali ya wasiwasi ilipozidi kulitokea nini? Kwa hivyo, utungo huu bado unahitaji kuegemezwa katika utungo mwengine ndipo ujumbe wake uweze kukamilika. Katika kishazi 'elezi cha hali' maana na msisitizo katika sentensi haubadiliki tunapohamisha nafasi ya kishazi hiki katika sentensi. Kutokana na matokeo haya kishazi hiki twaweza kusema kuwa, chaweza kuchukua uamilifu wa 'kirai elezi' katika sentensi kwa ukamilifu.

2.2.6 Kishazi elezi cha matokeo

Kishazi elezi cha matokeo huwa ni chagizo cha habari zinazotolewa. Hutoa maelezo zaidi kuhusu matokeo yaliyoko. Hebu tutazame mifano ufuatayo:

(ia) Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii ndiposa alipita mtihani.

Katika sentensi hii kishazi elezi kinatupatia maelezo ya matokeo ya kupita mtihani. Kefa alipita mtihani kwa kuwa alikuwa na nidhamu pamoja na kusoma kwa bidii. Matokeo ya kusoma kwa bidii na kuwa na nidhamu ni kufaulu katika mtihani.

(ib1) Ndiposa apite mtihani Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii.

(ib2) Ndiposa alipita mtihani Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii.

Maana ya sentensi hii ni sawa na ile ya sentensi (ia) Msisitizo nao u katika kule kupita mtihani.

*xyz_____

(ic1) Ndiposa Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii apite mtihani.

(ic1) Ndiposa Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii alipita mtihani.

Kishazi elezi cha matokeo kimetokea katikati ya kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu.

Sentensi imekosa mantiki. Huu sio muundo wa sentensi za Kiswahiki Sanifu.

(iia) Tulipanda maua kwa ustadi, kwa hivyo baraste ilipendeza sana.

Sentensi hii inaeleza matokeo ya kupanda maua.

*xyz_____

(iib1) Kwa hivyo baraste ilipendeza sana tulipanda maua kwa ustadi.

Sentensi haina mantiki.

(iib2) Kwa hivyo baraste ilipendeza sana, (kwa kuwa tulipanda maua kwa ustadi.

Sentensi imeleta mantiki tulipoongezwa kibainishi ‘kuwa’ na kitenzi cha kuwa ‘kuwa’.

Hii ni kumaanisha kitenzi hiki hakiwezi kutumika mwisho wa sentensi, kutokana na data tuliyonayo. Sentensi hii inaeleza matokeo ya baraste kuwa inapendeza.

*xyz_____

(iic1) Tulipanda maua kwa ustadi, baraste ilipendeza sana.

Huu sio muundo sahihi. Kwa kawaida sivyo tuzungumzavyo.

(iic2) (Kwa kuwa) tulipanda maua kwa ustadi, baraste ilipendeza sana.

Sehemu ya (kwa kuwa) ilipoongezewa sentensi ni kamili na sahihi. Sentensi hii inaeleza matokeo ya kupanda maua. Kishazi hiki kinachelea kubadilishwa nafasi katika sentensi.

2.2.7 Kishazi elezi cha namna/jinsi na ulinganishi

Kishazi hiki huwa na maneno ya kulinganisha hali, namna na jinsi mbili za vitu.

mambo na hali tofauti. Hebu tutizame sentensi zifuatazo.

(ia) Kama vile kipepeo huvutiwa na mwangaza, ndivyo Onyango alivyopendezwa na Gatwiri.

Katika sentensi hii kishazi elezi kinaeleza namna Onyango alivyopendezwa na Gatwiri. Tunao ufahamu wa jinsi kipepeo huvutiwa na mwangaza. Namna hiyo hiyo ndiyo inayolinganishwa na jinsi Gatwiri alivyompendeza Onyango.

*xyz_____

(ib) Ndivyo Onyango alivyopendezwa na Gatwiri Kama vile kipepeo huvutiwa na mwangaza.

Muundo wa sentensi unadhihirisha kuwa na mushkili. Hivyo basi inakuwa vigumu kuhamisha nafasi ya kishazi hiki.

*xyz_____

(ic) Ndivyo Onyango, kama vile kipepeo huvutiwa na mwangaza alivyopendezwa na Gatwiri.

Katika sentensi hizi, neno ‘ndivyo’ ni kielezi kilinganishi. Kinalinganisha kitendo cha Onyango cha kuvutiwa na Gatwiri na jinsi kipepeo anavyovutiwa na mwangaza. Katika muundo wa Kiswahili Sanifu kielezi hutanguliwa na kitenzi. Tunapotanguliza kielezi basi hukiuka muundo wa lugha hii. Hivyo basi sentensi hukosa mantiki. Data tuliyonayo haitoshelezi kuhitimisha kuwa kishazi elezi cha namna/jinsi na ulingnishi lazima kitokee mwanzo wa sentensi. Kutahitajika Utafiti zaidi kudhihirisha jambo hili. Lakini kwa hivi sasa tutachukulia kishazi elezi cha nama/ jinsi na ulinganishi kinapojitokeza katikati ya kiima na kiarifu sentensi hiyo hukosa mantiki.

(iia) Jinsi moshi upoteavyo angani, ndivyo ujana ulivyo!

Katika sentensi hii tunafahamu kuwa ujana ukishapita yaani mtu akizeeka, ujana hautarudi tena. Linalosisitizwa hapa ni jinsi moshi upoteavyo angani. Ujana ndio unaolinganishwa na moshi. Moshi ukishapaa angani hupotea. Ukishapotea haurudi tena wala hauwezi kupatikana tena.

(iib) Ndivyo ujana ulivyo, jinsi moshi upoteavyo angani.

Hapa sentensi tunaipata mantiki yake kwa umbali kidogo. Linalo sisitizwa hapa ni jinsi ujana ulivyo. Japo katika hali ya kawaida sivyo tunavyozungumza.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

*xyz _____

(iic) Ujana, jinsi moshi upoteavyo angani ndivyo ulivyo.

Kiima ndicho kimechukua nafasi ya kwanza ya sentensi.

Pia katika sentensi hii tunaipata maana ya sentensi. Kielezi kilinganishi 'ndivyo' kinapotenganishwa na kile kinacholinganisha, sentensi inaweza kukosa maantiki. Pia swala hili litahitaji utafiti wa kina. Mzungumzaji yeyote wa Kiswahili sanifu atahisi sentensi hii kuwa ina upungufu katika muundo wake.

2.2.8 Vishazi elezi vya kukubali

Vishazi hivi hujibu swali kama vile: hata kuweje? Hueleza kitendo kilichotendeka bila kujali hali, maelezo na hata mabadiliko yaliyofanywa ili kutokuweko kwa kitendo hicho. Mfano wa sentensi;

(ia) Alitamani sana kuhama japo nyumba ilikarabatiwa na wala kodi haikupandishwa.

TY

Mittins, W. H. (1962:105)

Linalosisitizwa hapa ni kule kuhama. Kuwa alikuwa ameshaamua kuhama hata kuje nini!

(ib) Japo nyumba ilikarabatiwa na wala kodi haikupandishwa alitamani sana kuhama.

Linalosisitizwa hapa ni jinsi juhudi zilifanywa za kumfanya abadilishe uamuzi wake. Lakini juhudi hizi hazikufua dafu. Hii ina maanisha sababu zake za kuhama sizo mwenye nyumba alizodhania kuwa sababu.

*xyz_____

(ic) Japo nyumba ilikarabatiwa alitamani sana kuhama na wala kodi haikupandishwa.

Hapa mzungumzaji anadhani labda mpangaji ana wasiwasi kuwa nyumba itapandishwa kodi kwa kuwa imekarabatiwa. Labda ndiyo maana ameamua kuhama.

(iia) Alikuwa tayari kuolewa na Jakobo ingawa Jakobo alikuwa kipofu.

Linalosisitizwa hapa ni kule kuolewa. Labda Jakobo alipata upofu baada ya kuwa na uchumba. Hakutaka kuvunja ahadi yake.

Alifahamu fika kuwa Jakobo alikuwa kipofu. Upofu huo haukuweza kumfanya kubadili chaguo lake.

(iib) Ingawa Jakobo alikuwa kipofu alikuwa tayari kuolewa na Jakobo.

Linalosisitizwa hapa ni upofu. Maana inayojitokeza hapa ni kuwa alimjua Jakobo akiwa kipofu. Alipokutana na Jakobo kwa mara ya kwanza Jakobo, alikuwa kipofu lakini alipoulizwa kama angaliolewa na Jakobo, alikubali. Upofu haukumzuia kuolewa na Jakobo.

*xyz_____

(iic) Ingawa alikuwa tayari kuolewa na Jakobo, Jakobo alikuwa kipofu.

Hapa linalosisitizwa ni kule kuwa tayari kuolewa na kipofu. Mzungumzaji hapa anajulisha msikilizaji kuwa Jakobo anayezungumziwa ni kipofu.

Labda msikilizaji hajawahi kujua Jakobo anayezungumziwa ni kipofu. Huenda ikawa pia anayeolewa hakuwa na ufahamu Jakobo ni kipofu.

2.2.9 Vishazi elezi vya nia/ kusudi

Vishazi hivi hujibu maswali kama vile: ni kwa kusudi gani? Umekusudia nini? Hutoa maelezo ni kwa nini kitendo kilitendeka. Mfano katika sentensi:

(ia) Ilibidi runinga ifungwe ili aweze kusikiliza kwa makini.

TY

Mittins, W (1962:105)

Ilipogunduliwa hakuwa anasikiliza kwa makini, kwa kutazama runinga, ilifungwa. Kusudi la kufunga runinga ni kuhakikisha umakinikaji wa kusikiliza.

(ib) Ili aweze kusikiliza kwa makini ilibidi runinga ifungwe.

Runinga ilifungwa ndipo mazungumzo yakaanza. Ilijulikana kama runinga itakuwa imefunguliwa hatasikiliza kwa makini.

*xyz _____

(ic) Ilibidi ili aweze kusikiliza kwa makini runinga ifungwe.

Alijulikana hatasikiliza kwa makini. Kwa hivyo, runinga ilifungwa kwanza ndipo mazungumzo yakaanza. Wazo la kufunga runinga huenda likawa lilitokana na msikilizaji mwenyewe. Hapa mzungumzaji hakujali kama wangaliweza kuendelea na mazungumzo huku wakitazama runinga.

(ia) Alitishia maisha ya watu ndiposa wakaamua kumpigia kura.

Watu hawakumpigia kura kwa hiari. Tisho walilotishiwa ndilo lilisababisha kumpigia kura.

*xyz _____

(ib) Ndiposa wakaamua kumpigia kura alitishia maisha ya watu.

Hata wakubali kumpigia kura ni kwa sababu ya tisho alilowapa.

*xyz _____

(ic) Ndiposa wakaamua alitishia maisha ya watu, kumpigia kura.

Sentensi hii haina mantiki. Inaonyesha kuwa kishazi elezi cha nia/ kusudi kinapotokea katikati ya kielezi kilinganishi na kitenzi, husababisha sentensi kutokuwa na maana. Japo hatuwezi kusema kuwa hili ni hitimisho. Data tuliyonayo haitoshelezi kuhitimisha jambo hili. Utafiti zaidi utahitajika kufanywa. Matokeo ya vielezi vilinganishi ‘ndivyo’ na ‘ndiposa’ ni sawa. Tazama [3.2.7, ib na ic,]

2.2.10 Vishazi elezi vya kiwango

Vishazi hivi hujibu maswali kama vile: jinsi? Kwa kiwango gani? Kiasi gani/kipi? na vipi? Hebu tutazame mfano wa sentensi:

(ia) Alisimama wima kana kwamba alikuwa ametengenezwa kwa jiwe.

TY

Mittins, W.(1967:106)

Kiwango kinachozungumziwa ni jinsi alivyosima. Hakuwa anasongea wala kutikisika ndipo kiwango cha kisimama kwake kikalinganishwa na jiwe.

(ib) Kana kwamba alikuwa ametengenezwa kwa jiwe, alisimama wima.

Kinachoangaziwa hapa zaidi ni kule kuwa kama jiwe. Kule kuwa kama jiwe, ndiko kulikomfanya kuonekana kusimama wima.

*xyz_____

(ic) Alisimama kana kwamba alikuwa ametengenezwa kwa jiwe wima.

kitenzi 'alisimama' na kielezi cha hali 'wima' hayawezi kutenganishwa. Sentensi ya tatu haina mantiki. Kutahitajika kiunganishi, hivi basi tutakuwa tunatoka nje ya mipaka ya utafiti huu.

(iia) Alimtandika rafikiye, mpaka akawa hajifahamu.

Kule kutojifahamu kunatueleza kiwango alichopigwa. Kinachoangaziwa zaidi hapa ni kule kupigwa.

*xyz_____

(iib) Mpaka akawa hajifahamu, alimtandika rafikiye.

Katika sentensi hii kutahitajika kiunganishi ‘ndivyo’, ndipo sentensi hii iweze kuwa na mantiki. Kama mtu ataweza kuelewa ilivyo, basi lazima kulikuwepo na mazungumzo ya namna hiyo hapo awali.

*xyz_____

(iic) Alimtandika mpaka akawa hajifahamu rafikiye.

Hapa sentensi inaeleweka moja kwa moja. Kuna mtu aliyemtandika rafiki yake kiwango cha kutojifahamu. Kinachoangaziwa hapa ni kule kumtandika. Sio kumtandika tu, lakini alimpiga mpaka akawa hajifahamu. Makubwa!!.

2.3 HITIMISHO

Kwa muhtasari, kuna aina mbalimbali ya vishazi elezi. Vilevile majukumu ya vishazi hivi ni mengi. Vishazi hivi hujitokeza mahali tofautitofauti katika sentensi. Wanaisimu wengi wamefafanua kishazi huku wakizingatia kuwepo kwa kiima na kiarifu.

Kutokana na vishazi elezi vyote nilivyofafanua, nimegundua ya kuwa hakuna kishazi elezi kisichokuwa na kitenzi. Hii inatuhitimishia kuwa hakuna tofauti kubwa iliyoko kati ya sentensi sahili na kishazi.

Matokeo ya kishazi kinapobadilishwa nafasi yake katika sentensi ni kuwa:

1. Msisitizo unaweza kuhama kutoka kwa kiima, na kwenda kwa yambwa au kitenzi. Kutoka kwa yambwa na kwenda kwa kiima au kitenzi. Pia kutoka kwa kitenzi na kwenda kwa kiima au yambwa.
2. Maana inaweza kubadilika kabisa.
3. Sentensi inaweza kupoteza maana na hata kukosa mantiki.
4. Maana ya sentensi hubaki ileile ya awali.
5. Kuna vishazi elezi visivyoweza kuchukua nafasi za virai elezi. Tunachukulia kishazi elezi kinapoteza maana yake kabisa, baada ya kubadilishwa nafasi yake katika sentensi, huwa kimeshindwa kuchukua uamilifu wa kirai elezi katika tungo husika.

SURA YA TATU

UTUMIZI WA NADHARIA YA X- BAA KATIKA

UCHANGANUZI WA VISHAZI ELEZI KWA

MUJIBU WA NADHARIA YA UMILIKIFU NA

MASHARTI

UTANGULIZI

Katika sura ya pili tuliainisha aina mbalimbali za vishazi elezi kwa mujibu wa wanaisimu kama: Household (1972), Quirk R. na Greenbaum (1973), Mittins, W.H. (1962), Polome, E. (1967), Jerono, P. (2005), Mwalili, M. N. (2008).

Kutokana na mchango wao, tuliweza kupata aina kumi tofauti ya vishazi elezi katika Kiswahili Sanifu. Katika sura hii, tutavichanganua vishazi aina zote hizi. Uchanganuzi wetu utaegemea nadharia ya X-baa kwa mujibu wa nadharia ya Umilikifu na Masharti (UM).


3.1 KISHAZI ELEZI CHA WAKATI

Katika sentensi (2.3.1 ia), 'Tangu tulipotoka Nairobi, mvua imekuwa ikinyesha sana', kielezi cha wakati 'tangu' ni KBn, 'tulipo-' ni sehemu iliyoambishwa kuonyesha wakati uliopita katika kitenzi '-toka'. 'Nairobi' ni KN kilicho na uamilifu wa mahali.

Walikotoka ni Nairobi. Sehemu ya KN inayotawaliwa na KU ni kapa. Hapa agumenti ni Nairobi. Kishazi hiki kinatuelezea muda mvua imekuwa ikinyesha.

Sentensi ya (2.3.1 iia), ‘Baada ya Kenya kunyakua uongozi kutoka kwa mbeberu, ufiisadi ulianza kutoa mizizi’, kishazi elezi cha wakati ni ‘baada ya Kenya kunyakua uongozi kutoka kwa mbeberu’. ‘Baada ya’ ni KBn kilicho na uamilifu wa kielezi cha wakati. ‘Kenya’ ni KN chenye uamilifu wa Kiima. ‘ku-’ ni sehemu iliyoambishwa kufanya kitenzi ‘-nyakua’ kuwa nomino/ kuwa katika hali yake ya uhalisia. Sehemu iliyobaki ni KN kilicho na uamilifu wa yambwa tendwa.

Kutoka sentensi ya (2.3.1 ia) kishazi elezi ‘ tangu tulipotoka Nairobi’ kielelezo chake ni kama kinavyodhihirishwa hapa chini:




xyz*

{-po-} ni kiambishi awali cha mahali.

3.2 KISHAZI ELEZI CHA MAHALI

Katika sentensi (2.3.2 ia), ‘Wasomi wa Kenya huenda kokote wanakothaminiwa kishazi
 ‘kokote wanakothaminiwa’ kitakuwa na kielelezo kifuatacho:



xyz*

{-po-} kiambishi awali cha mahali


'Kokote' ni KBn kinachotawaliwa na KKBn. Mofimu 'wa-' itachukuwa sehemu ya KN ikiwa na uamilifu yambwa tendewa. 'nako-' ni sehemu iliyoambishwa kuwakilisha kiima

katika kitenzi ‘-thamini-’ kilicho na uamilifu wa kiarifu. Mofimu ‘-wa’ itachukua sehemu ya KN inayowakilisha hali ya kufanyiwa. Virai nomino (VN) vyote viwili vilibebwa na kitenzi ‘-thamini-’. Katika sentensi (2.3.2 ii), ‘Pahali jumba lilichomeka, hatukuona lolote ila jimvu’. Katika kishazi, ‘Pahali jumba lilipochomeka’, kielezi ‘pahali’ kitachukua sehemu ya KBn. Nomino ‘jumba’ ni KN chenye uamilifu wa yambwa tendwa. Nomino ‘lilipochomeka’ ni KN chenye uamilifu wa yambwa tendwa. Kiima ni ‘moto’ lakini hakiko katika umbo bali katika umilisi wa wazungumzaji.

3.3 KISHAZI ELEZI CHA MASHARTI NA UKUBALIFU

Nomino ‘mgomo wa walimu’ imechukuwa nafasi ya KN chenye uamilifu wa kiima wakati umesababisha kutokuwa na masomo. Lakini yambwa pale unapotakikana kufutiliwa mbali na ‘chama cha walimu’ ambacho ndicho kiima. ‘kama’ imechukua nafasi ya KBn ‘hauta-’ ni sehemu ya kitenzi iliyoambishwa kukanusha kitenzi ‘kufutiliwa mbali’. Sehemu yote kutoka U,T ni kiarifu. Japo tukichukua neno ‘mbali’ likiwa peke yake katika utungo huu, litakuwa na uamilifu wa kielezi cha kitenzi ‘futiliwa’. Katika sentensi (2.3.3 ia), ‘Ingawa maisha yanachangamoto zake, lazima tukubaliane nayo’. ‘Ingawa na ‘yana’ ni vihusishi vinavyohusisha maisha na changamoto. ‘Maisha’ ni KN chenye uamilifu wa Kiima. Sifa ‘changamoto’ ni KN chenye uamilifu wa kiarifu. ‘zake’ ni kiwakilishi sifa.

Kutoka sentensi (2.3.3 iia) ‘Kama mgomo wa waalimu hautafutiliwa mbali na chama cha waalimu’, kielelezo chake ni kama kifuatavyo:



xyz*

ha- kiambishi awali cha ukamushi.


-u- kiambishi awali cha kiima.


-ta- ni kiambishi awali cha wakati.

Hebu tutazame sentensi hii.

‘Mary huenda anadhani kuwa atajiuzulu.’ Katika utungo huu kuna sentensi mbili nazo ni:

- (i) Mary huenda anadhani.
- (ii) Kuwa atajiuzulu.






Kielelezi hapa kimeishia na KT na wala sio KN. Itakuwa vyema tufahamu jambo hili. Sio lazima kila wakati kielelezo cha X-baa kumalizikia na KN.

'Mary' ni sehemu ya KN chenye uamilifu wa Kiima. Neno 'huenda' ni kitenzi kisaidizi cha kitenzi kikuu 'anadhani'. KBn 'kuwa' ni kitenzi cha 'kuwa'.

Tunapolinganisha na sentensi ya Kiingereza tunagundua kuwa muundo wa Kiswahili sanifu hauna Spesifaya. Hii ni kwa sababu, katika muundo wa Kiswahili nomino 'atajiuzulu' haibainishi wazi kama ni mwanamume au ni mwanamke. Katika Kiingereza, imebainisha wazi kuwa mtu anayezungumziwa kuwa atajiuzulu ni mwanamume. Katika Kiingereza wao husema: 'chairlady, chairman, wakati Kiswahili huzungumzia 'mwenyekiti'. Hapa mwenyekiti huyu hajulikani ni wa jinsia ipi. Haya ni maswala mapana yasiyokuwepo katika upeo na mipaka ya utafiti huu. kwa hivyo tutayawacha kidogo kisha tuangazie zaidi utafiti wetu. Tulitaka tu kuonyesha muundo wa lugha hizi mbili unavyotofautiana Kisintaksia.

3.4 KISHAZI ELEZI CHA SABABU

Katika sentensi (2.3.4 ia), ‘Nilimkopesha pesa kwa sababu alizihitaji’, kishazi ‘kwa sababu alizihitaji’, kitakuwa na kielelezo kifuatacho:




{-a-} ni kiambishi awali cha yambwa tendewa, kama aliyefaidi kutokana na kitendo 'kopesha'. Lakini kiima kutokana na kitendo 'hitaji'

Kwa kuwa vishazi vya aina hii huanza na kiunganishi, 'kwa sababu'. 'kwa' itachukuwa nafasi ya spesifaya, 'sababu' itachukuwa nafasi ya KBn. Sehemu ya KN itabakia kapa kwa kuwa kiima cha kishazi hiki kiko katika umilisi wa wazungumzaji. Kielezi 'alizihitaji' ndio KT chenye uamilifu wa yambwa tendewa pamoja na kiarifu. Mofimu 'a' inawakilisha yambwa inayozungumziwa katika kishazi hiki. Kitenzi 'hitaji' ambacho ndicho kinachoonyesha hali ya uhitaji aliokuwa nao, ndio kiarifu cha kishazi hiki. Katika umbo la kishazi hiki kiima hakiko. Wanasintaksia husema kuwa kiima hiki kiko katika umilisi wa mzungumzaji na msikilizaji. Kwa hivyo hakihitaji kutajwa. Hukosa kutajwa na mzungumzaji. Hii ndio maana hukosekana katika umbo. Ndicho kielelezo (4.6) hapo juu.

Katika sentensi (2.3.4 iia), Kwa vile Yusufu alipendwa zaidi na wazazi wake, ilibidi ahujumiwe na ndugu zake', kiunganishi kihusishi 'kwa vile' kinahusisha kitenzi 'kupenda' na wazazi wa Yusufu. Kiima ni 'wazazi' na kiarifu ni, 'alipendwa sana'. 'Yusufu' ni yambwa tendwa, yeye ndiye anayependwa sana na wazazi wake.

3.5 KISHAZI ELEZI CHA HALI


Katika sentensi (2.3.5 ia), 'Tulifunga safari tulipoona kuwa hali ya anga ilikuwa shwari', kishazi 'tulipoona kuwa hali ya anga ilikuwa shwari', kitakuwa na kielelezo kifuatacho:



KBn ‘kuwa’ kinadhihirisha utegemezi ulioko katika kishazi hiki.

Kiima katika kishazi hiki ni ‘hali ya anga’. Kimechukua nafasi ya KN kinachotawaliwa na KU. Kiarifu ni ‘shwari’. Nacho kimechukua nafasi ya KT inayotawaliwa na KT. Sehemu iliyoambishwa ni ‘ili-’ inayowakilisha wakati uliopita. Kitenzi kilichoambishiwa ‘ili-’ ni kitenzi cha ‘-kuwa’.

Hebu tutizame kishazi cha sentensi (2.3.5 iia), Raila alikubali kugawa mamlaka, hali ya wasiwasi ilipozidi’. Kishazi, ‘hali ya wasiwasi ilipozidi’, haina ‘KBn’. Kwa hivyo hatukuhitaji kielelezo cha ‘KKBn’. Kishazi cha kwanza kilihitaji sehemu ya ‘KBn’. Pia Kishazi cha kwanza kina nafasi ya KN. Lazima tungalianza na ‘KU’ ndipo tupate nafasi ya ‘KN’. Neno ‘ilipozidi’ limechukua umbo la ‘KN’ katika uamilifu wa kielezi cha kitenzi ‘wasiwasi’.




xyz*


{-po-} ni kiambishi awali cha mahali. kitenzi '-zidi' kina uamilifu wa kivumishi cha yambwa 'wasiwasi'.

3.6 KISHAZI ELEZI CHA MATOKEO

Katika sentensi (2.3.6 ia), ‘Kefa alikuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii ndiposa alipita mtihani’, Kishazi ‘Kefa alikuwa na nidhamu pamoja na kusoma kwa bidii’, nomino ‘Kefa’ imechukuwa nafasi ya KN kinachotawaliwa na KU.



VN vyote vinavyotawaliwa na 'T' vinauamilifu wa 'yambwa'. Vilivyo na uamilifu wa 'kiima' hutokana na 'T^l'.




Katika kishazi hiki, ‘kwa kuwa tulipanda maua kwa ustadi’, kiunganishi kihusishi ‘Kwa’ ni Spesifaya inayotawaliwa na KKBn¹. ‘kuwa’ ni kihusishi kinachohusisha uhusiano uliopo baina ya upandaji wa maua na matokeo yake ya baraste kupendeza. Kiima ni watu waliopanda maua. Wanawakilishwa na Mofimu ‘tu-’. Mofimu ‘tu-’ ni kiambishi awali kinachowakilisha kiima. Kiarifu ni sehemu ‘KT na KN’.

Katika kielelezo, mofimu ‘tu-’ na ‘li-’ ambayo ‘li-’ inawakilisha wakati na ‘tu-’ inawakilisha kiima zimeunganishwa na kuunda sehemu ya U, inayowakilisha sehemu iliyoambishwa ya kitenzi ‘panda’.

3.7 KISHAZI ELEZI CHA NAMNA/JINSI NA ULINGANIFU


Katika sentensi (2.3.7 na ii), ‘Kama vile kipepeo huvutiwa na mwangaza ndivyo Onyango alivyopendezwa na Gatwiri’ na Jinsi moshi upoteavyo angani ndivyo ujana ulivyo’, kishazi ‘kama vile kipepeo huvutiwa na mwangaza na cha pili, ‘jinsi moshi hupoteavyo angani’, kielelezo chake ni kama kinavyodhihirishwa hapa chini:

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION




3.8 KISHAZI ELEZI CHA KUKUBALI

Katika sentensi (2.3.8 ia), ‘Alitamani sana kuhama japo nyumba ilikarabatiwa na wala kodi haikupandishwa’. Kishazi, ‘japo nyumba ilikarabatiwa na wala kodi haikupandishwa’, kishazi hiki kina sentensi mbili. Kuanzia ‘na wala kodi haikupandishwa’ ndio sentensi ya pili. Hapa tunagundua ya kuwa, kishazi chaweza kuwa kikubwa kuliko sentensi. Kishazi kimoja kina sentensi tegemezi mbili. Katika uamilifu na hata umbo sentensi tegemezi yaweza kuwa ndogo kuliko kishazi elezi.



3.9 KISHAZI ELEZI CHA NIA/ KUSUDI

Katika sentensi (2.3.9 ia), ‘Ilibidi runinga ifungwe ili aweze kusikiliza kwa makini’, kishazi ‘ili aweze kusikiliza kwa makini’ kielelezo chake ni kama kinavyodhihirishwa hapa chini:



3.10 HITIMISHO

Tunapochanganua vishazi elezi kwa kutumia nadharia ya X-baa kwa mujibu wa nadharia ya Umilikifu na Masharti, matokeo tuliyopata ni kama yafuatavyo:

- (i) Kila kishazi elezi kilikuwa na sehemu ya kiima na kiarifu.
- (ii) Tumegundua ya kuwa kishazi kimoja chaweza kubeba sentensi tegemezi zaidi ya moja.
- (iii) Tunapokuwa na kapa katika umbo la kirai, agumenti hiyo huwa katika umilisi wa wazungumzaji.
- (iv) Hakuna kishazi elezi kilichokuwa na kitenzi kapa. Hii ni kumaanisha ya kuwa kila kishazi elezi kina kitenzi. Hivyo basi hoja hii ni muhimu kuongezewa katika maelezo na ufafanuzi wa dhana ya 'kishazi elezi'.
- (v) Katika kielelezo cha X-baa kishazi elezi chaweza kumalizikia katika KN au KT.
- (vi) Japo virai elezi vimeelezwa kuwa vitegemezi kuna virai elezi vilivyokosa Spes. wala KBn. Katika umbo la kishazi, sehemu hizi, ndizo hudhihirisha utegemezi wa vishazi elezi.
- (vii) Kirai nomino kinachotawaliwa na T ni yambwa.
- (viii) Kirai nomino kinachotawaliwa na T^1 ni kiima, kitenzi au kihusishi cha mahali.

SURA YA NNE

4.1 HITIMISHO

Katika utafiti huu, tuliahidi ya kuwa tutaainisha na kuchanganua vishazi elezi. Tumeviainisha vishazi elezi katika misingi ya uamilifu wake (wao) katika sentensi. Pia tumevichanganua vishazi hivi kwa kutumia njia mbili:

1. Vishazi hivi tulivihamisha nafasi zao katika sentensi husika. Yaani kwanza tuliviweka vishazi elezi mwanzoni mwa sentensi, mwishoni mwa sentensi na baadaye katikati mwa aidha kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu au katikati mwa kiima na kiarifu. Tulifanya hivi kupima ikiwa KE hubakia na maana pamoja na uamilifu wake kinapobadilishwa nafasi zake katika sentensi.

2. Kwa kuvichora katika kielelezo cha X-baa, tulividhihirisha katika vielelezo vya X- baa ili kubainisha kategoria amilifu za vishazi hivi.

Vishazi elezi vyote tulivyochanganua vina viarifu. Viarifu hivi ndivyo vinavyotueleza zaidi juu ya kitenzi kinachozungumziwa katika sentensi. Sio kila kishazi katika kielelezo cha X-baa kiima kilidhihirishwa katika umbo lake. Sio kuwa kuna kishazi kilikosa kiima

bali kinapatikana katika umilisi wa wazungumzaji. Kiima hiki pia huwa kimebebwa katika viambishi vya vitenzi.

Nafasi ya Spesifaya katika kielelezo cha X-baa:

Kila utungo ulio na Spesifaya huwa pia na KBn. Spesifaya yaweza kudondoshwa na kishazi kikawa bado kinajitosheleza. Lakini KBn kinapodondolewa kishazi hukosa mantiki. Hivi ni kumaanisha KBn ni muhimu katika tungo kuliko Spesifaya. Sio ajabu labda ndio maana Spesifaya kuwekwa ‘nje’ kabisa katika kielelezo cha X-baa. Kutokana na vishazi tulivyochanganua, hata Kiingereza Spesifaya sio ya lazima. Kishazi elezi chaweza kujitosheleza hata pale ambapo Spesifaya imedondolewa.

Baada ya kuainisha vishazi elezi, tumeweza kupata aina kumi. Aina hizi ni kama vile:

1. Kishazi elezi cha wakati: Hujibu swali kama: lini? Saa ngapi?
2. Kishazi elezi cha mahali: hujibu swali kama: wapi?
3. Kishazi elezi cha masharti na ukubalifu: hujibu swali kama, kwa nini?
4. Kishazi elezi cha sababu: hujibu swali kama, kwa nini?
5. Kishazi elezi cha hali: hujibu swali kama, vipi? Ilikuwaje?
6. Kishazi elezi cha matokeo: hujibu swali kama: Je, yalikuwaje? Vipi?
7. Kishazi elezi cha namna/ jinsi na ulinganifu: hujibu swali kama, vipi?
8. Kishazi elezi cha kukubali: hujibu swali kama, utafanyaje?

9. Kishazi elezi cha nia/ kusudi: hujibu swali kama, ni kwa kusudi gani? Una nia gani? Umekusudia nini?

10. Kishazi elezi cha kiwango: hujibu swali kama, gani?

Tumegundua ya kwamba tofauti zilizoko katika aina ya vishazi elezi hivi haziwezi kubainika wazi na kwa urahisi. Vishazi elezi tofauti huelekea kujibu swali moja. Kwa mfano: kishazi elezi cha sababu na kishazi elezi cha masharti na ukubalifu vyaweza kuchukuliwa kuwa sawa. Japo bado vinauamilifu tofauti katika muktadha.

Tofauti iliyoko ni kidogo sana kati ya kishazi elezi cha kiwango na kishazi elezi cha namna/jinsi na ulinganifu. Ni vyema ieleweke kuwa vishazi ninavyofananisha kimoja hakiwezi kutumika badala ya mwenzake katika sentensi. Ni kuvifananisha tu tunafananisha vishazi hivi. Vishazi elezi hufanana sana na virai elezi ambavyo si dondoshi. Tazama huu mfano ndipo tuweze kuelewa kufanana kulioko kati ya kirai elezi na kishazi elezi.

(i) Mwenye hatia alikaa mahali ambapo hangaliweza kuonekana. (kishazi elezi)

(ii) Mwenye hatia alikaa mafichoni. (kirai elezi)

Kirai elezi ‘mafichoni’ kinaeleza mahali aliko mwenye hatia.

Kishazi elezi ‘mahali ambapo hangaliweza kuonekana’ kinafafanua zaidi alikokuwa, hangeweza kuonekana.

Mahali _____ ni kiima.

Hangaliweza kuonekana _____ ni kiarifu.

Mafichoni _____ ni kielezi.

‘Kielezi’ na ‘kiarifu’ vimefanya kazi ileile katika sentensi: (i), (ii).

Kwa hivyo tutahitimisha kuwa kiarifu katika kishazi elezi ndicho hufanya kazi moja na kirai elezi kutokana na data hii

4.2PENDEKEZO

Katika kuufanya utafiti huu, tumekumbana na changamoto mbalimbali, tumejaribu kutatua baadhi ya changamoto hizi lakini nyingine hatukuweza kuzitatua kwa sababu ya kujikita katika mipaka ya utafiti huu. Kutokana na matokeo ya utafiti tungependa kupendekeza utafiti wa kishazi elezi ufanywe tena. Uchanganuzi wa kishazi elezi ufanywe kwa kutumia nadharia ya theta. Hii ni kwa sababu tulipobadilisha nafasi ya kishazi elezi katika sentensi, tuligundua kwamba maana na mkazo wa ujumbe ulibadilika. Nadharia ya theta itafaa ili kupata maelezo zaidi kwa kutumia agumenti za kishazi husika.

MAREJELEO

Abdulaziz, M. H., (1996), *Transitivity in Swahili*. Rudigen Copper Verlag, Koln.

Brondal, (1972), *The Problem of Hypotaxis*, In *Syntactic Theory 1: Structuralist*:

Householder (ed.), Harmondsworth: Penguin.

Bussman, H (1996), *Routledge Dictionary of Language and Linguistic*. Routledge, London.

Chomsky, N. (1957) *Syntactic Structures*. The Hague

Chomsky, N. (1965), *Aspects of the Theory of Syntax*, Cambridge, Mass.

Crystal, (2003), *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*; Oxford: Blackwell.

Haegeman, L. (1991), *An Introduction to Government and Binding*: Cambridge University Press.

Haegeman, L., (1991), *An Introduction to Government and Binding Theory*: Oxford: Blackwell Publishers.

Haegeman, L., (1995), *The Syntax of Negation Cambridge*: Cambridge University Press.

Householder, W. Fred, (1972), *Syntactic Theory I: Structuralist*. Penguin Books Ltd. Harmondsworth, England.

Householder, W. Fred, (1972), *Syntactic Theory I: Structuralist*: Penguin Books Ltd:
Harmondsworth: England.

Jerono, p. (2005) *Kishazi Huru cha Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu cha
Nairobi. (Haijachapishwa).

Kapinga, M. C (1983), *Sarufi Maumbo Kiswahili Sanifu*. TUKI, Dar es Salaam.

Leech. G. na Svartvik, J., (2000), *A Communicative Grammar of English 2nd Ed.*
Longman. London.

Massamba, D. P. B. et al, (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na*
Vyuo: Dar es Salaam: Tuki.

Massamba, D. P. B. et al, (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondary na Vyuo*
Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu R. S., (1990), *The Structure of Swahili Sentences: A Transformational Approach.*
Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Nairobi: (haijachapishwa).

Mgullu, R. S, (1990), *The Structure of Swahili Sentence: A Transformational Approach:*
Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu cha Nairobi (

Mittins. W. H., (1962), *A Grammar of Modern English*: Newcastle: Methuen and CCo.
Ltd.

Mutua, J. N. (2005), *Kishazi kitegemezi cha Kiswahili: Mtazamo wa Sintaksia ya X-baa*
Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi: (haijachapishwa).

- Olali, T. M. (1997) *Kikundi Nomino cha Kiswahili. Mtazamo wa Sintaksia ya X-baa*.
Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu cha Nairobi. (hajachapishwa)
- Polome. E., (1967), *Swahili Language Handbook*: Washington D.C: Center for Applied
Linguistics.
- Quirk, R. na S. Greenbaum, (1973), *A University Grammar of English*: Sussex Longman.
- Quirk, R. na S. Greenbaum, (1973), *A University Grammar of English*: Sussex:
Longman.
- Quirk, R. na wenzake, (1972), *A Grammar of Contemporary English* London:
Longman.
- Radford, A. na wenzake, (1999), *Linguistics: An Introduction*: Cambridge: Cambridge
University Press.
- Richards. J. na wenzake, (1985), *Dictionary of Applied Linguistics*. Longman, Harlow.
- Swaleh, R. H., (2005), *Mofosintaksia ya Kishazi cha Kitikuu*: Mtazamo wa Uminimalisti.
Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu cha Nairobi: (hajachapishwa).
- Tuki, (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha Dar es Salaam*: Tuki.
- TUKI, (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*: Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI, (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*: Dar es Salaam: TUKI.
- Tuki, (2006), *English Swahili Dictionary 3rd Edition*: Dar es Salaam Tuki.

TUKI, (2006), *English-Swahili Dictionary 3rd Edition*: Dar es Salaam: TUKI.

Vitale, A., (1981), *Swahili Syntax*: Holland Foris Publications.

Weber, H. (1985) *A Dictionary of Phonetics and Linguistics*. Harlow. Longman.